# Pambazuko

Toleo Namba 083 | Jumatatu, Agosti 5 - 11, 2024

Fuatilia mfululizo wa makala za Afcon kila Jumatatu ukurasa wa 33 | Gazeti Maalum la Afcon 2027


## Mwabukusi ataka majaji kuchunguza utekaji Uk. 15

# Zanzibar yavuruga Katiba ya Jamhuri




**Leo hii ukisoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano bado kuna nafasi ya waziri kiongozi, je, huyo waziri kiongozi yupo? Jibu ni hapana,"**

● Wastaafu, wadau wakemea

Habari Uk. 6

## Soma Ndani

### Ruto 'ararua' upinzani, ODM yaweweseka



Soma zaidi Uk. 26

### Mbatia amuonya Samia, ashauri abadilike

**RAIS Samia Suluhu Hassan adaiwa kuzungukwa na wasaidizi wasiomweleza ukweli wala kumtakia mema....**

Soma zaidi Uk. 12

## Canada yampa kongole Samia

### >Balozi Kyle Nunas agusa DP World

**JITIHADA na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan kuitumikia Tanzania, yamepongezwa na Canada na kuhimiza kuimarishwa ili umma upate maendeleo...**

Soma zaidi Uk. 4



*Balozi wa Canada nchini Tanzania, Kyle Nunas akizungumza na Mhariri Mkuu wa Pambazuko, Simon Mkina wakati wakisafiri kwa treni ya kisasa kuelekea Dodoma kwenye uzinduzi wa huduma za reli inayotumia umeme (SGR), uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan wiki iliyopita. (Na mpiga picha wetu).*

## Tahariri/Katuni

# Ni hatari kumomonyoa Muungano

HABARI kuu katika gazeti la leo - la Pambazuko Agosti 5 2024, inazungumzia kukiukwa kwa misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mmoja wa washirika wa muungano huo wa nchi mbili; Tanganyika na Zanzibar.

Anayebainishwa na habari hiyo kukiuka misingi ya Katiba hiyo, ni Zanzibar, kwamba imethibitika pasi na shaka kuwa nchi hiyo imekiuka baadhi ya misingi muhimu inayounda Jamhuri.

Kimsingi, yanayotajwa kukiukwa na Zanzibar, yamo kikatiba, na yamejengwa tangu kuasisiwa kwa makubaliano ya kuwepo kwa muungano huo miaka 60 iliyopita.

Kwamba mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar yaliyofanywa mwaka 2010, hayana "baraka za mshirika mwenza" – ambaye ni Tanganyika, kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Habari hiyo, imeandikwa kwa umakini mkubwa kwa kupitia vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuoanisha na mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar, ambayo yalianza kutekelezwa baada ya kuridhiwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.


Mbali na kuzichambua katiba zote mbili, gazeti hili la Pambazuko limepata maoni ya wabobezi wa sheria na katiba, wakiwamo pia viongozi waandamizi wastaafu ndani ya serikali ya sasa na zilizopita, ambao wote wanaeleza namna msingi iliyoasisiwa na Muungano huo, kusiginwa.

Ni kutokana na mazingira hayo, Pambazuko linahimiza kuendelea kuheshimiwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili muungano wetu – wa mfano duniani, uimarike zaidi na kuleta matunda yanayotarajiwa.

Kukiuka na hata kumomonyoa sehemu hata moja ya Katiba ya Jamhuri, ni kuhatarisha maendeleo, umoja, mshikano na ustawi wa wananchi wa nchi hizo mbili zilizoamua kuungana Aprili 26, 1964.

Pambazuko linahimiza kuwa ni vyema na haki, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuheshimiwa na pasitokee mshirika yeyote ndani ya muungano huo kukengeuka kwa sababu zozote zile.

Mungu ibariki Tanzania na watu wake wote.



# Rais akiteta na mwl. wake



*Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na mwalimu wake aliyemfundisha Chuo cha IDM Mzumbe (Sasa Chuo Kikuu Mzumbe) Sabina Geleja mara baada ya hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa kampasi mpya ya chuo hicho jana. (Picha na Ikulu)*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**


## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mhariri wa Habari** | : | Maregesi **PAUL** | 0689 732 325 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

Habari Kuu

# Canada yampa kongole Samia



*Balozi Kyle Nunas*

Na Mwandishi WETU

JITIHADA na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan kuitumikia Tanzania, yamepongezwa na Canada na kuhimiza kuimarishwa ili umma upate maendeleo zaidi.

Pongezi hizo zimetolewa na Balozi wa Canada nchini Tanzania, Kyle Nunas wakati akihojiwa na Pambazuko mwishoni mwa wiki kuhusu masuala anuai, ikiwamo miradi ya kimkakati, demokrasia na vyombo vya habari.

Mazungumzo ya Balozi Nunas na mwandishi wa Pambazuko yalifanyika ndani treni ya kisasa inayotumia reli ya umeme (SGR) kutoka Dar es Salaam kuelekea Dodoma.

Safari hiyo iliyoongozwa na Rais Samia, ilikuwa maalum kwa ajili ya kuzindua rasmi huduma za treni na reli hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa wa maendeleo ya Tanzania.

Pambazuko linaweka mahojiano hayo katika mfumo wa maswali na majibu ya Balozi Nanus;

**Pambazuko:** Tunatambua kwamba wiki mbili zijazo utakuwa unamaliza muda wako wa kazi Tanzania na kurejea Canada, je, ni nini kinachokufurahisha kwenye uongozi wa Rais Samia?

**Balozi:** Aksante sana kwa kupata nafasi ya kukaa nawe ndani ya treni  hii mpya, ambayo ni matunda ya kazi ya viongozi wa Tanzania, lakini hasa Rais Samia ambaye amekuja kuhitimisha na sasa inafanya kazi.

Yapo mambo mengi sana ambayo mimi binafsi napenda kuona yakiendelezwa zaidi na Rais Samia na hata viongozi wengine wanaokuja.

Rais Samia ni kiongozi anayechapa kazi, anajali utu, anathamini na kusikiliza wengine, anafanya kazi kubwa kuleta maendeleo ya Tanzania.

Siwezi kusema kila kitu, kwa kuwa viko vingi, lakini nafurahi kumuona Rais Samia anatenda haki zaidi na kuacha watu wakiwa huru zaidi.

**Pambazuko:** Umekaa Tanzania miaka miwili sasa, umeona idadi ya wawekezaji, wakiwamo kutoka Canada ikiongezeka, je, uwekezaji unasaidia nchi au ni aina nyingineya unyonyaji?

**Balozi:** Katika mazingira ya sasa, hakuna nchi, hata zile tajiri, zinazoweza kufanya kila kitu, ikiwamo biashara kubwa, hivyo wawekezaji makini ni lazima ili nchi isonge.

Katika Tanzania, wa-Canada ni miongoni mwa wawekezaji wakubwa katika sekta ya madini, hawa pamoja na wengine wanasaidia nchi kupiga hatua na kamwe siyo wanyonyaji kama wengine wanavyoweza kufikiri.

Karibuni tulishuhudia Tanzania ikiingia mikataba ya kuendesha baadhi ya sehemu katika Bandari ya Dar es Salaam na Kampuni ya DP World, na kulikuwa na kelele nyingi, lakini ukweli ni kwamba uwekezaji ule ukisimamiwa vyema, utakuwa na manufaa makubwa kwa Tanzania na nchi zinazoizunguka.

Nimeona kuanza kwa matunda kwenye uwekezaji ule, kwamba sasa meli kubwa zilizoshindwa kutia nanga, sasa zinakuja na hiyo maana yake ni kwamba mizigo mingi itaingia na mapato ya nchi yatakuwa makubwa zaidi.

**Pambazuko:** Unaondoka karibuni kurejea Canada, je, unatamani kurudi ukiwa mgeni wa hadhi ya utalii? Umependa zaidi vivutio gani?

Inaendelea Uk. 6

Jicho la Tai

# Rais Samia, siyo chakula tu, hata uonevu utaibua vijana wa GenZ

Na Igo Al

MTANZANIA mwenye umri wa miaka 81, anayejitambulisha kuwa ndiye raia halali wa Tanzania, akiitwa Mzee Tai, ameibuka na kumuongezea jambo Rais Samia Suluhu Hassan.

Mzee Tai, ameandika waraka kwa umma na kuupitisha mezani kwa mhariri wa Pambazuko, akitaka umfikie Rais Samia, lakini pia usomwe na umma.

Katika waraka wake wa kurasa 11, Mzee Tai ameandika mengi, akianza na pongeza kwa Rais Samia, kwamba anafanya kazi nzuri ya kuongoza vyema Tanzania.

Mzee Tai anamsifu kiongozi huyo wa Tanzania kwamba "anaupiga mwingi" katika kuleta neema kwa wananchi, na kueleza kuwa Rais Samia halali usiku wala mchana akihangaikia wale alioita "vijana wake" ili waishi maisha mazuri.

Katika waraka huo, Mzee Tai pia amegusia kauli ya Rais Samia aliyoitoa wiki iliyopita, wakati akizindua bwawa kubwa la kumwagilia miwa la Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, Morogoro.

Akiwa huku, Rais Samia alisema ni vyema uzalishaji wa sukari, na mazao mengine ya chakula ukaongezwa, kwani kukosekana kwake, kunaweza "kuingiza vijana barabarani."

Kwamba vijana hao wakikosa chakula, wanaweza kuanziaha maandamano ambayo yana rangi ya vurugu, wakidai kupata chakula na kuwa watafanya lolote ili wasife kwa njaa.

Mzee Tai akaongeza jambo kwa maono hayo ya Rais Samia, kwamba siyo chakula tu na sukari, vijana hao, maarufu kama GenZ, wanaweza kuingia barabarani kudai kuwepo kwa demokrasia ya kweli.

Hakukomea hapo, akasema GenZ wakiona wanaonewa sana, hasa na vyombo vya dola, wanaweza kujikusanya na kuamua kuelekea makazi rasmi ya Rais Samia kudai kutendewa haki, ikiwa hawaipati sehemu zinahohusika.

Mzee huyo akasema ni vyema Rais Samia akafanya kila analoweza sasa kuhakikisha vijana wa GenZ hawaingii barabarani - kama ilivyotokea Kenya, kwa kuhimiza serikali yake kutenda haki, kuacha kuminya demokrasia na zaidi sana kukomesha rushwa.

"Namuasa Rais Samia, asidhani ni njaa tu ya chakula ndiyo itawaingia GenZ barabarani, bali kuonewa, kuminywa kwa haki na kukosekana kwa usawa, kutawaingiza barabarani," alimaliza Mzee Tai kwenye waraka wake.

## Tutumie tafsiri yako ushinde...




***Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri fupi, inayoelezeka na kufafanua vyema kuliko zote na itachapishwa na gazeti hili kwenye Ukurasa wa 30 toleo linalofuata. Mhusika atatumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263 .***

Habari Kuu

# Z'bar yavuruga Katiba ya Jamhuri

Na Waandishi WETU

MABADILIKO ya Katiba ya Zanzibar na utendaji wa serikali ya visiwa hivyo, kunavuruga na hata kuvunja misingi ya kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwamba mabadiliko hayo ya Katiba ya Zanzibar yanaonekana kuipa nguvu zaidi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika baadhi ya maeneo ya msingi.




Hayo yameelezwa na baadhi ya viongozi wastaafu, wanazuoni, wanasiasa na wachambuzi wa katiba, wengi wakiwa wanasheria wakati wakizungumza na Pambazuko, huku wakishauri kurekebishwa kwa mazingira hayo ya kukengeuka kwenye misingi ya Katiba ya Muungano.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilifanya marekebisho ya Katiba ya visiwa hivyo na kuridhiwa na Baraza la Wawakilishi, na kuanza kutumika 15 Septemba, 2010.

Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ziliungana kwa kufunga mkataba wa Muungano Aprili 26, 1964 na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wote walizungumza na Pambazuko wamesisitiza kuwa nchi zote mbili zilizoungana

Inaendelea Uk. 7

# Canada yampa kongole Samia

Inatoka Uk. 4

**Balozi:** Lazima nitarejea Tanzania, napenda watu wake, ni wakarimu na kuna vivutio vingi. Unajua mimi ni mtaalamu wa kupiga picha. Katika matembezi yangu mbugani, ambako nimeenda mara kadhaa, nimepiga picha zaidi ya 1000 nzuri. Hakika nitarudi hapa kutembea.

**Pambazuko:** Vitu gani vikubwa unaondoka ukiwa unasikitikia Tanzania na watu wake?

**Balozi:** Ninaondoka nikiwa na masikitiko makubwa kuhusu ajali za barabarani. Hizi zinamaliza watu wengi sana na nimeona sababu kubwa ni kutokuwa na madereva makini au wale wenye ujuzi wa kazi hiyo.

Wakati naenda kuwasilisha hati zangu kwa Rais Samia kule Dodoma, sikupata ndege, tukaamua kwenda kwa gari, lakini njiani sikuwa na amani hata kidogo, madereva, hasa wale wa magari makubwa na yale ya abiria walikuwa wanaendesha hovyo. Hiyo ndiyo sababu kubwa ya ajali.

Natamani kusikia siku moja Tanzania ajali zimepungua, nitafurahi sana.

**Pambazuko:** Unazungumziaje uhai wa demokrasia na uhuru wa vyombo vya habari Tanzania?

**Balozi:** Kuhusu demokrasia, nimekuwa nikifuatilia hata kabla sijafika Tanzania nikiwa balozi, hivi sasa naona mambo ni mazuri, siasa zinafanyika kwa uhuru, hasa mikutano ya vyama vya siasa. Zamani naambiwa vilizuiwa. Sasa naona wanasiasa wanafanya kazi zao vyema.

Vyombo vya habari navyo vinafanya kazi vyema, nakumbuka zamani kulikuwa na "fungia-fungia" ya magazeti, kwa kuwa nadhani serikali haikupenda wananchi wajue nini hasa kinaendelea kwa watendaji na viongozi, lakini sasa naona mnaandika bila woga.

Serikali na viongozi wake wanapaswa kuelewa kuwa vyombo vya habari ni uhai wa taifa, bila ninyi kuandika na kukumbusha viongozi namna bora ya kuwatumikia wananchi, basi nchi inaweza kuharibika.

**Pambazuko:** Chakula gani cha Tanzania ambacho unatamani kuendelea kukipata hata ukiondoka?

**Balozi:** Tanzania mmebarikiwa kuwa na aina nyingi ya vyakula tofauti na huko kwetu, ambako unaweza kula chakula cha aina moja tu kwa muda mrefu.

Mimi sikuwa mpenzi wa ugali, ambacho ni chakula kikuu hapa Tazania, lakini nilipenda zaidi kutafuna mishikaki.

Habari

# Z'bar yavuruga Katiba ya Jamhuri

Inatoka Uk. 4

zinapaswa kuheshimu Katiba Kuu ambayo ni ya Jamhuri ya Muungano, ili kuendelea kuimarisha muungano huo.

Balozi Karume akemea

Mwanasiasa mkongwe kutoka Zanzibar, Balozi Ali Karume, ameliambia Pambazuko kwamba mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar, yamevunja misingi ya Muungano, hivyo kuwa chanzo cha baadhi ya watu kunung'unika kwamba Muungano umetikiswa.

Amesema Katiba ya Zanzibar iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010, inabeba maeneo kadhaa ambayo yanapishana na misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


Balozi Karume amesema kimuundo, Katiba ya Zanzibar inamezwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo jambo lolote linaloundwa na kufanyika nje ya matakwa ya Katiba ya Muungano, linakuwa batili.

"Ni wazi, wote tunajua kuwa mkiunda kitu chochote ambacho kinakuwa kinyume na Katiba ya Muungano, hicho kitu kinakuwa batili, kwa hiyo kama kuna kitu kinaundwa kinyume na matakwa ya Katiba hiyo, hakiwezi kuwa na uthabiti..."

"Hii inatokana na tafsiri yangu kwamba Katiba ya Zanzibar imemezwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa sababu inazungumzia nchi ambayo ni Jamhuri ya Muungano na Zanzibar ambayo ni nchi, lakini ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano..."

"Na ndiyo maana hapa Zanzibar tuna marais wawili, huyo mmoja Rais wa Zanzibar anashughulikia mambo yote ya Zanzibar iliyopo ndani ya Muungano, na huyu wa pili Rais wa Jamhuri ya Muungano..."

"Huyu wa pili ambaye ana haki ya kushuka Zanzibar saa yoyote akawaita viongozi wa Jeshi, viongozi wa Polisi, viongozi wa Usalama, lakini anawaita wote hao kwa sababu hivyo ni vyombo vya Muungano na mkuu wake ni yeye..."




"Lakini huyu hawezi kuthubutu kufika Zanzibar akawaita watu wa Kilimo, Maliasili au mambo mengine ya Zanzibar ambayo hayamuhusu na akifanya hivyo, atakuwa anakosea," ameongeza balozi huyo mstaafu.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaainisha kwenye Ibara ya 64(3) kuwa; 'Endapo sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inahusu jambo lolote katika Tanzania Zanzibar, ambalo liko chini ya mamlaka ya Bunge, sheria hiyo itakuwa batili na itatanguka na pia endapo sheria yoyote iliyotungwa na Bunge inahusu jambo lolote ambalo liko chini ya Mamlaka ya Baraza la Wawakilishi, sheria hiyo itakuwa batili na itatanguka.'

Balozi Karume amesema Katiba ya Zanzibar iliyobadilishwa ikaleta Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) mwaka 2010, ni kweli imepigiwa kura ya maoni Zanzibar na kupitishwa Zanzibar, lakini haikutiwa kwenye Katiba ya Muungano, kwa kuwa haikupelekwa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muun-

Inaendelea Uk. 8

rifaly
Habarika kidijitali! Soma gazeti la Pambazuko na magazeti mengine maarufu kwenye Rifaly!
Scan to download Rifaly
www.rifaly.com

Habari

# Z'bar yavuruga Katiba ya Jamhuri

Inatoka Uk. 4

gano wa Tanzania kwa ajili ya kuridhiwa.

"Sasa hili suala ni la kupelekwa mahakamani kwamba Katiba ya Zanzibar imeingiza vifungu ambavyo havijatambuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, lakini ile Katiba ya zamani vifungu hivyo vilitambuliwa na Katiba ya Muungano," amesema.

Anaeleza kuwa Katiba ya Muungano ina sehemu nne; ya kwanza inazungumzia urais, ya pili inazungumzia bunge, ya tatu inazungumzia mahakama na ya nne inazungumzia Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kuna mtu aliniuliza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mbona inakinzana na Katiba ya Zanzibar, nikamwambia katika nchi yoyote ya Muungano, ukiona katika yoyote inakinzana na ile ya Muungano, basi ujue Katiba ya Muungano ndiyo inatawala.

"Hapa kwetu, Katiba ya Muungano inaeleza wazi kuwa kule Zanzibar kutakuwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, kutakuwa na Waziri Kiongozi, lakini huku kwenye mabadiliko inaonesha kuwa kutakuwa na Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili..."

"Inaelekeza kuwa Rais atatoka kwenye chama kinachotawala na Makamo wa Kwanza atatoka kwenye chama cha upinzani kinachoongoza kwa kura, na Makamo wa Pili ndiye anayepewa dhamana ya kuongoza na kuendesha nchi endapo itatokea lisilotegemewa," amefafanua.

Balozi Karume amesema kuwa mmoja wa waasisi wa muungano huo, Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanzania, aliwahi kuonya kuwa watu wasichezee Katiba, kwani kuna madhara makubwa kufanya hivyo, ikiwamo kuleta mifarakano.

Amehimiza kujitokeza vyombo vya habari na taasisi nyingine kusema kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imevurugwa, hivyo kutaka kuwepo marekebisho ili Muungano uendelee kuimarika.

**Dkt. Slaa anena**

Mwanasiasa wa siku nyingi, ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dkt. Wilbroad Slaa amesema kwa sasa inaonekana kwamba Katiba ya Zanzibar imeondoa mamlaka mengi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Zanzibar.

> **"Kila rais anayekuja anaondoka, akiondoka anakuwa ameshaharibu kwenye eneo hilo na kuliharibia taifa, anaendelea na maisha yake huku akiacha amewagonganisha Watanzania. Hakuna anayejali," alisema Dkt. Slaa.**

Amesema kutokana na mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar, sasa nchi hiyo imejijengea himaya ya kujisimamia na kujitegemea kana kwamba ni dola.

"Katiba kubwa (ya Muungano) inazungumza rais ana mamlaka ya kugawa mikoa, umewahi kusikia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatangaza wakuu wa mikoa na wilaya wa Zanzibar? Sasa faida yake nini kuwa nayo kwenye Katiba?

"Ni wazi kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sasa haiangaikiwi, ni kwamba inavyoonekana, hii Katiba ivunjwe ama isivunjwe, inaonekana ni sawa tu..."

"Kila rais anayekuja anaondoka, akiondoka anakuwa ameshaharibu kwenye eneo hilo na kuliharibia taifa, anaendelea na maisha yake huku akiacha amewagonganisha Watanzania. Hakuna anayejali," alisema Dkt. Slaa.

**Butiku atoa ya moyoni**

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Mwalimu Nyerere (MNF), Joseph Butiku, amesema pamoja na kuwepo kwa mabadiliko kadhaa, "yenye nia njema" kwenye Katiba ya Zanzibar, yalipaswa kufanyika kwa utaratibu unaokubalika.

"Pamoja na kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo yamekuwa yakifanyika kwa nia nzuri na njema, ni vyema kuhakikisha kuwa yanafuata utaratibu ili kuondoa kasumba ya kupuuza Katiba

Inaendelea Uk. 14

## Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



# Israel, Iran ziangalie zaidi usalama wa dunia

MAUAJI ya kiongozi wa kundi Hamas la Palestina, Ismail Haniyeh, huko Tehran nchini Iran yameibua hofu za mgogoro mkubwa kati ya Iran na Israel.

Kulingana na taarifa za habari, kiongozi mkuu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei, ametoa amri ya mashambulizi ya moja kwa moja dhidi ya Israel.

Hatua hii inaashiria kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa kulipiza kisasi kutoka kwa Iran.

Mvutano huu umepandishwa hadi kiwango cha juu zaidi kutokana na historia ya migogoro kati ya Iran na Israel, pamoja na msaada wa Iran kwa vikundi vya upinzani katika eneo hilo.

Kwa mfano, Aprili, mwaka huu, Iran ilifanya mashambulio makubwa dhidi ya Israel, na sasa inaweza kutumia mauaji ya Haniyeh kama kichocheo cha hatua zaidi.

Kwa upande mwingine, Israel imejipanga vizuri kukabiliana na vitisho kutoka Iran kwani ina jeshi lenye uwezo mkubwa na imekuwa ikifanya mazoezi ya kijeshi kwa ajili ya kukabiliana na mashambulio yanayoweza kutokea.

Pia, Israel imekuwa ikishirikiana na washirika wake katika eneo hilo na kimataifa katika jitihada za kuzuia hatua za Iran.

Athari za mgogoro huu zinaweza kusambaa mbali zaidi ya eneo la Mashariki ya Kati. Kuna hatari ya kuongezeka kwa ghasia katika eneo hilo, pamoja na uwezekano wa kuongezeka kwa mgogoro kwa kushirikisha nchi nyingine.

Pia, mgogoro huu unaweza kuathiri usalama wa kimataifa, hasa kwa kuwa Iran na Israel zina silaha za kisasa, ikiwemo silaha za nyuklia.

Jumuia ya kimataifa ina jukumu muhimu katika kuzuia mgogoro huu kuongezeka. Ni muhimu kwa nchi zinazokuwa na ushawishi katika eneo hilo, kama vile Marekani, Urusi, na China, kushirikiana katika jitihada za kudumisha amani na kuzuia hatua za kijeshi.

Kwa ujumla, mauaji ya Haniyeh yameibua hali ya wasiwasi mkubwa katika eneo la Mashariki ya Kati.

Kadhalika, Iran italazimika kuchukua hatua sio tu kwa minajili ya kulipa kisasi, bali kulinda hadhi yake ndani na nje ya nchi hiyo, hasa kwa vile kufanikiwa kwa mauaji hayo kumesabisha nchi hiyo kudhihakiwa kwamba ni chui wa karatasi (paper tiger) yaani inaonekana kuwa taifa lenye nguvu lakini, dhaifu.

Ni muhimu kwa pande zote kuchukua hatua za kuzuia mgogoro huo ili kuhakikisha kuwa vita vinaepukwa wa manufaa ya raia.

Iran na Israel zinapaswa kutambua kuwa kuruhusu vita kati yao, ni kuhatarisha usalama wa dunia pia, kwani nchi marafiki zinaweza kuingilia na hatimaye kuleta tishio kubwa la vita kubwa zaidi.


Nchi hizo ni vyema kuimalisha ushirikiana katika jitihada za kudumisha amani na usalama.

***https://instagram.com/evarist_chahali***



Tafakuri ya Bagonza

# Ukiishi muda mrefu utaona Mwabukusi wengi



*Wakili Boniface Mwabukusi wakati akiapishwa kuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), katika ukumbi wa Jakaya, jijini Dodoma. (Picha na Mwananchi)*

Na Dkt. Benson BAGONZA

WANYAMBO wenye hekima husema; “bora uporwe mali kuliko kuzeeka, kwa sababu ukiporwa mali, marafiki zako wanaweza kukuchangia ukawa na mali tena.”

Mimi sasa ni mzee na nimewahi kuona “vi-Mwambukusi” na “ma-Mwambukusi wengi.”

Hawa, tena baadhi yap niliowaona, ninawataja ikiwa ni rejea ya safu yangu ya leo;

Kwanza nilimwona Julius Kambarage Nyerere. Waingereza “wakamMwambukusi” kuwa ni mchochezi. Akahukumiwa. Faini ikalipwa. Ikawa jioni, ikawa asubuhi, akawa rais wa kwanza wa Tanganyika. Waingereza wakapiga saluti, bendera yao ikashuka, ya “Mwambukusi” ikapanda.

Pili, nilimwona Madiba Mandela wa Afrika Kusini. Makaburu “WakamMwambukusi” kuwa ni gaidi. Miaka 27 akanyea debe, na alipoomba maji ya kunywa, askari jela mmoja alimpa mkojo anywe. Ikawa jioni, ikawa asubuhi. Mandela akawa rais. Akakutana mgahawani na askari huyo aliyempa mkojo. Akamkaribisha mezani kula naye. Askari akatokwa  jasho katikati ya baridi kali.

Tatu, kuna mmoja simtaji jina. Akakamatwa na polisi wa usalama barabarani. Akabambikiwa makosa ya usalama barabarani.

Akapewa kebehi. Akaambiwa ang’atwe na mbu kwa kuwa mbu wana haki ya kupata chakula. Leo ni rais wao. Askari wanampigia saluti. Akisinzia ndani wanalala nje kumlinda. Akikohoa, wanampongeza kwa afya njema. Hicho ndicho kisasi bora kuliko vyote.

Namwamini Yesu Kristo. Huyu walim-Mwambukusi mpaka kaburini. Akafufuka, wakamsujudia na kuishi naye.

Mitume wote, manabii wote - hakuna aliyeepuka u-Mwambukusi. Achana na hawa mitume wetu wasiotumwa na yeyote. Puuza hawa manabii wetu wasio na unabii, bali wamejawa na uhitaji.

Sasa Mwambukusi ndiyo habari ya mjini. Siyo wa kwanza kuwa Rais wa TLS na kamwe hawezi kuwa wa mwisho.

Nampongeza. Nina neno naye. Asiogope kujaribu kutikisa mbuyu, lakini pia asiogope kushindwa. Kwa nini? Waliomtesa ndio wahanga wa kesho wa mfumo uleule.

Katika enzi hizi ni “Ni hatari kuwa sahihi wakati serikali imekosea”. Bora ukosee wakati serikali iko sahihi.

Penye haki wote tuko salama. Penye dhuluma hakuna aliye salama. Asubuhi waweza kupigiwa makofi na saluti; jioni ukapigwa makofi na kurushwa kichura.

Mwalimu Nyerere alimwambia Mandela alipokuja Tanzania. “You are not free; you are out of jail.”- kwamba hauko huru, ni kwamba umetoka tu lupango. Mfumo ni kitu cha hatari. Kina tabia ya kuwala hata waliokiunda.

Msimuharibie Mwambukusi. Namwona ana uwezo wa kujiharibia. Leo twampenda sote; kuna siku tutamchukia wote. Hakuna umaarufu wa kudumu. Inayodumu ni haki.

Kwetu sote wana na mabinti wa Tanzania, tupendane.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjili Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

# Kampeni ya Tutunzane isiishie Morogoro

NILIKUWA miongoni mwa waandishi waliohudhuria hafla iliyofanyika Agosti 3, 2024, pale uwanja wa Sokoine uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Morogoro wakati Rais Samia Suluhu Hassan akizindua kampeni ya "Tutunzane" yenye lengo la kukomesha migogoro inayozuka mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji katika mkoa huu.

Uzinduzi huo uliwakutanisha vinara wa matukio ya migogoro wakiwakilisha pande zote mbili za wakulima na wafugaji kwa kupeana mikono mbele ya mkuu huyo wa nchi.

Juhudi za Rais Samia kuzindua kampeni ya "Tutunzane" ni za kupongezwa. Ni wazi kwamba bila kuwepo kwa amani na usalama, maendeleo yanayotarajiwa hayawezi kufikiwa.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba vita na migogoro vinapoteza muda mwingi na rasilimali ambazo zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo.

Hivyo basi, jitihada hizi zilizofanywa na viongozi wa Mkoa wa Morogoro zinapaswa kuungwa mkono na kila mmoja wetu.

Hata hivyo, kuna maswali muhimu yanayojitokeza; je, tatizo la migogoro kati ya wakulima na wafugaji ni kukosekana kwa kampeni kama hii ya "Tutunzane"?

Iwapo kampeni hii itafanikiwa kuzima migogoro hii, je, itakuwa na uwezo wa kutekelezwa katika maeneo mengine nchini na kufikia matokeo chanya kama ilivyo Mvomero?

Wakati tukitafakari majibu ya maswali hayo, ebu tujipe muda wa kuangazia chanzo cha kuibuka na hatimaye kushamiri kwa migogoro kati ya wakulima na wafugaji

Migogoro kati ya wakulima na wafugaji ina sababu nyingi; moja ni ukosefu wa ardhi ya kutosha. Ieleweke kuwa wakulima na wafugaji, wote wanahitaji ardhi kwa ajili ya shughuli zao, lakini inapokuwa ndogo na kukosekana kwa usimamizi wa matumizi, basi mifarakano hutokea.

Pia ukosefu wa mipango miji na vijiji nayo ni sababu nyingine kwani kunakosekana mipango thabiti ya matumizi ya ardhi, hivyo kuleta mwingiliano wa shughuli za kilimo na ufugaji.

Kitu kingine ni ukosefu wa elimu na uelewa, kwamba wakati mwingine, migogoro inatokana na ukosefu wa kutambua njia bora za kushirikiana na kutumia ardhi kwa pamoja.

Jambo la jingine linaweza kuwa ni ukosefu wa rasilimali za maji, kwani wakulima na wafugaji – wote wanahitaji maji kwa shughuli zao. Ukosefu wa rasilimali hii muhimu husababisha vita vya kugombea maji.

Ikiwa kampeni hii itafaulu Mvomero, ni muhimu ifanyiwe tathmini ili kuona kama inaweza kutekelezeka maeneo mengine nchini Tanzania.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba migogoro kati ya wakulima na wafugaji haipo Morogoro pekee, bali ni tatizo la kitaifa.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***



*Rais Samia Suluhu Hassan*

Habari

# Mbatia amuonya Samia, ashauri abadilike

Maregesi PAUL na Arodia PETER

RAIS Samia Suluhu Hassan adaiwa kuzungukwa na wasaidizi wasiomweleza ukweli wala kumtakia mema, ndiyo maana "mambo mengi hayaendi sawasawa."

Madai hayo yametolewa na Mwenyekiti wa zamani wa Chama cha NCCR- Mageuzi, James Mbatia, kwenye mahojiano maalum na gazeti la Pambazuko nyumbani kwake, Mbezi Beach, Dar es Salaam, wiki iliyopita.

Kutokana na kuwepo kwa watu hao, Mbatia ameshauri Rais Samia kuwa nao makini, kubadilika na kuchukua hatua haraka ili kunusuru taifa.

"Nasema hivyo kwa sababu kwa sasa Rais Samia amezungukwa na watu wanaompotosha katika uongozi wake, ndiyo maana hali si shwari nchini..."

"Hebu jiulizeni, yale maridhiano na Chadema yameishia wapi? Yale mambo ya kikosi kazi yameishia wapi? Nawaambia kuna watu wanampotosha Rais Samia ndiyo maana mnaona mambo hayaendi, yaani kuna kukamiana kwingi kila mahali, amesema Mbatia.

Mbatia ametahadharisha kwamba iwapo Rais Samia hatachukua hatua haraka kukabiliana na matatizo makubwa yanayotokea nchini – ambayo huenda mengine hapewi taarifa sahihi, basi Tanzania inaweza kupoteza sifa nyingi ambazo imekuwa nazo kwa muda mrefu.

Amesema ikiwa mambo mengi yanayolalamikiwa na wananchi hayatapatiwa ufumbuzi, huenda kampeni za uchaguzi mkuu zijazo, zitatumika fedha nyingi kwa ajili ya kudhibiti watu, badala ya fedha hizo kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo.

**Atabiri upinzani kushinda**

Akizungumzia uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani unaotarajia kufanyika mwakani – 2025, Mbatia ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Vunjo, amesema vyama vya upinzani vina nafasi kubwa ya kushinda wakati wa uchaguzi huo.

"Vyama vya upinzani bado vina nafasi kubwa ya kupata ushindi kwenye uchaguzi huo kwa sababu Watanzania sasa wanavielewa na kuviamini, kinachotakiwa ni kuwepo kwa uhuru, uwazi na haki..."

"Upinzani umekuwa tishio kwa chama tawaka,

Inaendelea Uk. 22



*Mwenyekiti mstaafu wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, (katikati) akizungumza na wahariri wa gazeti la Pambazuko, Maregesi Paul (kushoto) na Arodia Peter wakati wa mahojiano maalum yaliyofanyika nyumbani kwake Mbezi Beach, Dar es Salaam hivi karibuni. (Picha na Fidelis FELIX)*

## Kona ya Dkt. Bisimba



Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA

# Kiswahili kisiachwe kiharibike kwa makosa

KATIKA jambo ambalo naona linafanyika vibaya na hakuna mtu au mamlaka inayojaribu kutafuta ufumbuzi, ni matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili.

Kwamba kuna makosa katika matumizi ya irabu a, e, i, o na u yanapochanganywa katika matumizi na konsonanti kama ha, he, hi, ho, hu, na pia matumizi ya l na r.

Makosa hayo yameenea nchini ilihali lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya taifa yenye hadhi ya kutumika katika Jumuia ya Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika.

Tanzania husemekana kuwa kitovu cha lugha hii.

Jambo linaloshangaza ni namna Kiswahili kinavyotumika kiholela nchini kwa maana kuwa kuna watu wengi katika kuongea na hata katika maandishi, hufanya makosa ya kisarufi na hata ya kuchanganya herufi kwa kutumia irabu badala ya konsonanti na kinyume chake.

Hili ni jambo la ajabu sana kwa jamii ambayo inadaiwa kuwa kitovu cha lugha hiyo.

Katika mjadala niliokutana nao katika kundi moja kwenye mitandao ya kijamii, ni matumizi ya irabu na konsonanti na matumizi ya r na l.

Mara nyingi, baadhi ya watumiaji wa Kiswahili wanaweka r sehemu ya l, ama anaweka l sehemu ya r. Kwa mfano reli atasema leli.

Badala ya kalamu atasema karamu na kwa bahati mbaya siyo katika kusema tu, unaweza kukuta hii ikijitokeza hata kwenye maandishi kwenye vyombo vya habari kama magazeti na televisheni ambavyo vina wahariri.

Haiishii hapo. Kuna maneno ambayo yakichanganywa huleta maana tofauti kabisa. Kama vile kalamu na karamu.

Kwa upande wa kuchanganya irabu na konsonanti, wapo watu ambao wanapata shida ya matumizi ya neno lenye konsanati h badala yake wanaweka irabu kama vile a, e, i, o na u.

Huweza kuweka h ambapo hapastahili au kuiondoa ambapo inastahili. Mfano mtu anaandika 'Baba hatakuja', wakati akimaanisha 'baba atakuja'.

Unaweza kukuta tangazo limeandikwa 'mkutano umehairishwa' badala ya 'mkutano umeahirishwa.'

Katika mjadala huo, mmoja wetu aliafiki kuwa Kiswahili chetu ni kibovu na akawalaumu waandishi wa habari akitoa mifano akisema unaweza kukuta imeandikwa 'abari' badala ya 'habari' 'afazali badala ya 'afadhali', 'tafazali badala ya tafadhali' , 'zambi badala ya dhambi' 'uzuru badala ya udhuru' na mengine mengi.

Ni bahati mbaya sana haya yanaachwa yakiendelea vivyo bila kurekebishwa kiasi kuwa baadhi yanakaribia kuonekana kama ni maneno sahihi ya Kiswahili.

Ni vyema wahariri wa vyombo vya habari wajipambanue katika hili na kushika nafasi zao kama walinzi wa lugha.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***



*Mwalimu akiwa darasani mkoani Kagera. (Picha na Mtandao)*

Habari

# Z'bar yavuruga Katiba ya Jamhuri

Inatoka Uk. 8

ambayo ikiendelezwa, mwisho wake hauwezi kuwa mzuri," amesema Butiku.

Butiku amesema katika nyakati hizi ambazo nchi inaongozwa kwa mujibu wa Katiba, jambo lolote linalotolewa uamuzi nje ya utaratibu wa kikatiba, linaweza kufanyika na kutekelezwa, japokuwa mwisho wake ni kuendekeza utaratibu wa kutosheshimu Katiba.

"Kwa utaratibu wa kikatiba, kama inatakiwa kubadili jambo lolote kwenye Muungano, kunatakiwa kufuate Katiba inavyosema. Swali, je, mabadiliko yote yaliyotokea kuanzia mazungumzo yaliyozaa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar (SUK) na mengine yaliyofanyika, yalizingatia Katiba? Sasa jibu ni ndiyo au hapana, watu wanadadisi na kufuatilia..."

"Kwa wanaofahamu watasema yalizingatia Katiba. Watasema kifungu hiki, kama kinasema viongozi wa serikali wanaweza kuzungumza yakaisha, sawa..."

"Kama kifungu kinasema lazima Katiba izingatiwe, kifungu cha Katiba kilichozingatiwa ni kipi? Sasa ukifika hapo ndiyo watu wanasema mbona ule Muungano uliokusudiwa na waasisi siyo huu," ameongeza.

**James Mbatia naye**

Mwenyekiti wa zamani wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia amesema kuwa mabadiliko makubwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 2010, yameivuruga Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kwa lugha ya kisheria tunaweza kusema wamefanya makosa makubwa ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.."

"Ingawa wao walifanya jambo kubwa la maendeleo yao, wakaifanya Zanzibar ikatulia, fujo zote zilizokuwa zinatokea zikatulia, wakaja na serikali yao ya Umoja wa Kitaifa, lakini wameivuruga kabisa Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa hatua hiyo kwa kuwa uamuzi huo haukufika na kupitishwa na Bunge la Jamhuri..."

"Leo hii ukisoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano bado kuna nafasi ya waziri kiongozi, je, huyo waziri kiongozi yupo? Jibu ni hapana," ameshangaa!

Katiba ya Jamhuri inaainisha kupitia Ibara ya 105(1) ikisema; 'Kutakuwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar litakalokuwa na wajumbe wafuatao: (a) Mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi; (b) Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.'

Hata hivyo, mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 2010 yanaeleza katika Ibara ya 39 (1) kuwa; 'Kutakuwa na Makamo Wawili wa Rais ambao watajuilikana kama Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais.'

Mbatia anasema jambo hilo la mabadiliko ya viongozi wakuu wa Zanzibar, bado halijarekebishwa katika Katiba ya Muungano na kusababisha mgongano huo mkubwa.

"Sasa swali ni je, Rais wa Muungano ana mamlaka tena na Zanzibar?" anahoji Mbatia.

Msimamo wa Jaji Warioba

Waziri Mkuu (mstaafu), Jaji Joseph Warioba, amekuwa miongoni mwa viongozi wanaohoji sababu hasa za Zanzibar kuamua kufanya mabadiliko ya Katiba na kuanza kutumika bila kupata ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mara nyingi, akiwa katika mialiko amekuwa akizungumza uhalali wa Zanzibar kuamua kuchukua dhamana ambazo zinapaswa kufanywa na uongozi wa Muungano, bila kuelezwa kwamba kumekiukwa Katiba.

"Wenzetu kule (Zanzibar) tunawaona wanafanya mambo yao tu, tena mengine yanayotakiwa kutambuliwa na Jamhuri, sasa tunajiuliza, wamepata wapi mamlaka hayo," alihoji Jaji Warioba, katika moja ya hafla jijini Dodoma, hivi karibuni.

Mwanasheria Mkuu wa Tanzania, Dkt. Eliezer Feleshi, hakupatikana kuzungumzia jambo hili na kutoa msimamo wa serikali, kwani mara zote simu yake iliita bila kupokewa.

**"Wenzetu kule (Zanzibar) tunawaona wanafanya mambo yao tu, tena mengine yanayotakiwa kutambuliwa na Jamhuri, sasa tunajiuliza, wamepata wapi mamlaka hayo," alihoji Jaji Warioba, katika moja ya hafla jijini Dodoma, hivi karibuni.**

# Mwabukusi ataka majaji kuchunguza utekaji



*Kitendo cha utekaji.*

Na Andrew MSECHU

RAIS wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Boniphace Mwabukusi ameshauri kuundwa kwa Tume Huru ya Kijaji kuchunguza matukio ya utekaji.

Amesema kuendelea kushamiri kwa matukio ya utekaji, utesaji na mauaji, hakuonyeshi umakini wa serikali katika kuwalinda watu wake.

Akizungumza katika mahojiano maalumu na kituo cha luninga cha Star TV usiku wa Jumamosi Agosti 3, 2024, alisema vitendo hivyo vya kijinai vinadhalilisha Tanzania.

Mwabukusi ambaye alitangazwa mshindi Urais wa TLS Ijumaa Agosti 2, mwaka huu alisema Rais Samia Suluhu Hassan anapaswa kuchukua hatua ya kuunda tume hiyo kwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni anaonekana kushindwa kuwajibika.

"Waziri Masauni hajawajibika, na kauli yake ni ya kubeza maumivu waliyopata Watanzania, ni kauli iliyokosa utu na kwa kauli hii, mimi binafsi nimuombe Rais samia aunde Tume huru ya Kijaji..."

"Tume hii ichunguze hao wanaodaiwa kuwa wanajiteka, kujing'oa meno na kujipiga risasi, tujue wanajiteka wapate raha gani, kuna raha gani katika kujiteka, kujing'oa meno, kujipiga risasi na kujitesa,"alisema.

Mwanasheria huyo alisema kuna mazingira ambayo nchi inahitaji tume huru ya kijaji kuchunguza madhara ya utekaji yalivyo na kupata suluhisho lake.

"Leo unamsikiliza Masauni anazungumza kama vile mambo ni mepesi, nadhani ajipe utulivu aangalie kuhusu ukubwa wa dhamana aliyopewa na Rais Samia, kwa sababu wakati fulani watu watakuwa wanaingia kwenye chuki dhidi ya rais, lakini ni kutokana na picha mbaya na kauli na kutokuwajibika kwa wasaidizi wake, aliowakabidhi dhamana," alisema.

**Uongozi wake TLS**

Mwanasheria huyo aliweka wazi kwamba katika uongozi wake ndani ya TLS hataacha ujasiri na hataruhusu hofu iwe sehemu ya maisha yake, kwa sababu hakuna binadamu aliyeumba uhai, kwa hiyo hana haki ya kutoa uhai.

"Uhai ni zawadi ninayoipata kwa Mungu na huko ndiko ninakoweka maisha yangu mimi, taifa langu nitalisimamia bila hofu, sehemu ya kukemea nitakemea, sehemu ya kuonya nitaonya, sehemu ya kushauri nitashauri, kwa sababu kuna makaburi mengi tunayapita huko barabarani siyo wote walikosoa au walipigania haki za watu, ikifika wakati wako, umefika tu, lakini lazima tuishi maisha yetu kwa faida..."

"Mimi ninachojua ulinzi wangu mkubwa ni Mungu ninayemwamini na kusimama katika kweli, kama kuna gharama ninayohitaji kuilipa kwa sababu nimesema ukweli, basi nitailipa nikitabasamu," alisema.

Mwabukusi alisema hakuna haja ya watu kuwa na hofu na uongozi wake, huku akiwataka wadau kuondoa shaka inayotokana na desturi na tabia iliyojengeka ya watu kutokuwa wakweli.

"Nchi yetu haijazoea kurekebisha, ukimuona mtu anaiba mali ya umma mwambie wewe ni mwizi wa mali ya umma wala siyo tajiri, wala usitoe msaada na hata kama ni kanisani akileta sadaka mfukuze, ni mwizi kama mwizi mwingine," liongeza Mwabukusi.

Ana kwa Ana

# Maandamano ni kupoteza muda -Mzee Butiku



*Askari wa Kenya akifyatua bomu la machozi kama sehemu ya kuwadhibiti raia waliojitokeza kwenye maandamano nchini humo. (Picha na RFI)*

Na Mwandishi WETU

JULAI 12, mwaka huu, gazeti la Pambazuko kilipata fursa ya kufanya mahojiano maalumu na Mkurugenzi wa Mfuko wa Malimu Nyerere (MNF), Joseph Butiku ambaye alizungumzia mambo muhimu katika taifa.

Katika sehemu ya kwanza iliyotoka Jumatatu - Julai 15, 2024, Butiku alizungumzia mtazamo wake kuhusu yanayoendelea nchini Kenya na mambo mengine.

Leo tunachapisha maswali na majibu, huku Butiku akisifia uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan katika kuiweka Tanzania salama na yenye manufaa. Endelea…

**Swali:** Utendaji wa Rais Samia unatathminiwa, na kupatikana kwa maoni tofauti, kwa uzoefu na mtazamo wako unauonaje uongozi wake?

**Jibu:** Ukiangalia katika baadhi ya masuala unajua huyu mama, kwa maoni yangu, anakwenda vizuri. Amerithi nchi katika msiba, naye alikuwa makamu.

Mimi nadhani Rais Samia alianza vizuri na anakwenda vizuri na hasa katika maeneo matatu anayokwenda nayo. Moja, tunazungumza. Siyo kwamba hapo zamani tulikuwa hatuzungumzi.

Wakati wote watu wa magazeti mlikuwa mnazungumza. Nchi hii haijafungwa kuzungumza tangu enzi za Baba wa Taifa (Mwalimu Julius Nyerere).

Lakini Rais Samia amepanua wigo wa mazungumzo na amesema Watanzania tuzungumze, vyama tuzungumze tena mzungumze yale yaliyoko mioyoni mwenu, ili tuyajue kwa sababu tukiyajua tutajua namna ya kusaidiana.

Pili, amewasikiliza wanasiasa na vyama vyao. Wengine hawajaridhika, lakini yale makubwa waliyokuwa wanayataka, kwa mujibu wa hali halisi ya nchi hii, amewapa.

Madai kuhusu uchaguzi wa rais amewapa, tume huru ya uchaguzi amewapa, mikutano ya hadhara amewapa, sasa siku hizi unamuona kiongozi mmoja wa upinzani anakusanya watu, anafanya mikutano barabarani, anakutana na watu wake, anafanya maandamano japo mimi siyakubali, maana hayasaidii mtu.

**Swali:** Unamaanisha nini unaposema huyakubali maandamano?

**Jibu:** Maandamano kwangu hayana maana, jenga hoja na wale wenzako mfanye kitu, mpate jibu la hicho mlichokuwa mnakitaka.

Maandamano ni mtindo wa wanyonge. Walianza Waingereza huko katika chama cha Labour kwa sababu walinyang'anywa ardhi yao.

Maandamano haya ni katika mfumo wa vyama vingi. Sisi Waswahili hatukuwa na mfumo wa vyama vingi, watu kwa maeneo na makabila yao, walikuwa na machifu, tena mkipita raia wanaanguka chini, wanawasujudu machifu na sidhani kama hiyo attitude (tabia) hiyo imebadilika sana.

Sasa tumetoka huko, tuko kwenye vyama vingi. Mfumo wa vyama tulio nao ni ule wa Waingereza. Wakati wa mapinduzi ya viwanda huko Uingereza, hao waliokuwa na nafuu, waliwanyang'anya wenzao wote ardhi wakabaki bila ardhi.

Kwa hiyo, wasio na ardhi wakatengeneza kundi lao wakaliita chama cha Labour. Kwa hiyo hivi

Inaendelea Uk. 17

Ana kwa Ana

# Maandamano ni kupoteza muda -Mzee Butiku

Inatoka Uk. 16

vyama ni vyama vya kudai walichonyang'anywa.

Sisi tulikuwa tunamdai mkoloni na tukafanikiwa, baada ya hapo ni vyama vya kujenga.

Mtawala ameshaondoka sasa unamdai nani? Vyama vya siasa ni vyama vya kusaidiana na lazima iwe hivyo, kusaidiana kuboresha utaratibu wa uongozi na kuendesha nchi kwa manufaa ya Watanzania.

Haviwezi kuwa vyama vya ugomvi, maandamano, wakati watu wetu ni maskini. Ni kupoteza muda.

**Swali:** Lakini maandamano yanaruhusiwa kisheria, kikatiba?

**Jibu:** Sheria wakati mwingine tunaangalia, siyo mnaiga sheria za wazungu na hii imeingia vichwa vya wasomi, kuiga tu sheria za wazungu, hakuna common sense (maarifa ya kawaida).

Nani anayetengeneza Katiba? Mimi ningekuwa rais, ningeibadili, tuzungumze twende mbele tusipoteze muda, watu wetu ni maskini mno.

Niwaambie na mtafakari, wakati tulipokuwa na chama kimoja, mnajua tulianza na vyama vingi wakati wa utemi, ukawa ugomvi tu hapa.

Mimi ninavyojua, na nilikuwepo, mafanikio yote ya nchi hii mnayoyaona, yalikuwa kwenye chama kimoja. Wote tulikubaliana, japokuwa hatukukubaliana kila kitu, lakini tulikwenda na tulikuwa masikini hatuna elimu.



**Swali:** Unatamani tuachane na mfumo wa vyama vingi?

**Jibu:** Kwa suala la mfumo wa vyama vingi, tuendelee navyo kwa sababu ni mfumo. Maoni yangu ni kwamba mfumo huu ni wa fujo.

Niambie tangu uanze umefanya kazi inavyopasa?

Tumefanya uchaguzi mara ngapi, vyama vingapi vimepita? Kwenye uchaguzi uliopita, kama ungekuwa mfumo ambao mnauelewa na mnauamini, ulifanya kazi gani? Ulileta malalamiko? Kwa nini? Umeleta ajira kiasi gani? Umeleta maji? Umeleta viongozi wangapi?

**Swali:** Lakini ulileta sauti…

**Jibu:** Wewe una sauti kiasi gani? Hata watu watu wa press (magazeti) mna sauti kiasi gani? Mimi najua, siku zote mnachotaka kusema hakiishi, mnataka uhuru, uhuru, mnataka uhuru gani? Uhuru wa vyombo, sasa mnao mmekuja kuniuliza maswali.

Vyama vingi mimi nataka kabisa viwepo, lakini kazi yao siyo magomvi kama tunayoshuhudia. Wanaweza kuwa wanatofatiana, lakini wanatakiwa kufikia hatua ya kukubaliana kuzungumza kama watu wazima, hasa kuhusu taifa lao na kuboresha.

Hawatakubaliana wakati wote, lakini wasipokubaliana wajue kuwa kanuni moja ya vyama vingi ambayo ni suala la majority rule (uongozi wa wengi).

Lazima mtabishana ila mtafika mahali wengi wakiamua mnakubali, ilimradi tumpate nafasi ya kusema kuwa lakini mlivyofanya nadhani sivyo, siyo kuzuia maendeleo.

Swali: Kuna jambo umegusia kuhusu Katiba, umesema ungekuwa Rais ungebadili hii katiba.

**Jibu:** Mimi nilikuwa kwenye Tume ya Katiba, ninawauliza, tulihangaika na katiba ile, mnayo sasa?

Katiba ya sasa inasema hakuna wizi, hakuna rushwa, hakuna

Inaendelea Uk. 18

## Ana kwa Ana



*Vijana wa Gen Z wakiwa kwenye maandamano jijini Nairobi, Kenya.*

# Maandamano ni kupoteza muda -Butiku

Inatoka Uk. 17

uonevu. Katiba hii imeegemea kwenye misingi ya chama cha Tanu na ukiifungua inasema binadamu wote ni sawa.

Kama hatuba ya Nyerere ya mwaka 1962 il-ivyosema kuwa tunataka kujenga taifa la watu wenye usawa, taifa la watu huru, wote tupate maendeleo.

Ukisoma Azimio la Arusha linasema hivyo hivyo, lilitengenezwa kwa sababu kuna wengine wanataka kuwa matajiri sana na kuwanyima wengine, kwa hiyo tusema watu wote twende na tuweke misingi.

Tuliweka misingi. Misingi yote hiyo inazingatia Katiba ambayo inasema nchi hii ni yetu wote. Madaraka yote yanatoka kwa wananchi.

Pili tuko hapa kujenga usawa, uhuru, demokrasia na nchi hii itaendeshwa na vyama, kwa hiyo tunaruhusu vyama viendeshe nchi hii.

**Swali:** Kwa hiyo hakuna haja ya katiba?

**Jibu**: Kasoro kubwa iko wapi? Sema kasoro ipo sema tuizungumze.

Tulijaribu kufanya hapa kitu ambacho watu walitaka, walitaka serikali tatu. Sisi tukasikiliza, tukaleta maoni ya serikali tatu.

Zanzibar walitaka serikali tatu. Tukaenda kwenye mapendekezo, wakakataa.

Lakini kinachoonekana, Zanzibar wanavunja katiba, hivi hamjui Zanzibar wanavunja Katiba? Mimi sijawahi kusema lakini hivi ninyi mnaweza kusema hivi? Si mna uhuru wa kusema?

Tatizo ninyi ni waoga kupita kiasi, hamtetei haki zenu. Ni wabinafsi na mtu mbinafsi analinda sana nafsi yake, hawezi kupata shida ili wenzake wapate.

Kungekuwa na watu akina Nyerere hawa, tunajua kwa nini Nyerere aliacha kazi na akaamua kuhangaika na hata akatoka hana kitu katika nchi hii.

Lakini ninyi siku hizi mnashindwa. Rushwa hii nani anakula? Hivi unaweza ukasema kuwa hii nchi ni kwa sababu ya rushwa siwezi kwenda kugombea ubunge?

Nitakwenda kwenye chama tu kwanza au tutaunda kingine na kusema hiki chama si cha rushwa na utahangaika hata wakikupiga mkong'oto?

**Swali:** Shida kubwa ni nini katika suala hili la kubadili katiba?

**Jibu:** Katiba inatengeneza mfumo wa sheria na haki na sheria inalinda ubinafsi wa mtu. Maana ya kuwa na sheria inamaanisha inasimamia ubinafsi, kwa hiyo inajenga mimi ya mtu.

# Serikali kudhibiti udanganyifu mitihani vyuo vikuu nchini

Na Adonis BYEMELWA

SERIKALI imejipanga kuhakikisha kuwa hakuna udanganyifu wowote unaoweza kufanywa kwenye matokeo ya mitihani ya vyuo vikuu.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, hivi karibuni alisema utendaji wa mifumo ya mitihani katika vyuo vikuu nchini, uko salama, lakini serikali inafuatilia kwa ukaribu kuwepo kwa taarifa za udanganyifu.

Profesa Mkenda alieleza kuwa wizara yake ina mpango wa kuhakikisha mifumo ya mitihani inaangaliwa kwa kina baada ya kutokea tuhuma za rushwa zinazohusiana na kubadilisha alama za wanafunzi.

"Tumezisoma tuhuma hizi kwenye gazeti kwamba kuna wanafunzi wanahonga ili matokeo yakishaingizwa kwenye mfumo wa Tehama yabadilishwe," alisema Profesa Mkenda.

"Kuliwahi kutokea tuhuma kama hii katika chuo kimoja, lilitajwa jina la mwanafunzi na mtu aliyehusika kubadilisha hayo matokeo. Nilimwagiza katibu mkuu aunde tume huru ya uchunguzi, ikiwa ni pamoja na Idara ya Usalama wa Taifa na wataalamu wa Tehama, waliingia kuangalia mfumo wote..."

"Uzuri ni kwamba ukiingia kwenye mfumo ni lazima itaonekana uliingia saa ngapi na mabadiliko yapi yamefanyika. Uchunguzi ulipokamilika iligundulika siyo kweli, bali kulikuwa na vita ya kimamlaka inaendelea ndani ya chuo kile, hivyo waliamua kuchafuana," alisema Prof. Mkenda.

Hata hivyo, waziri huyo alisisitiza kuwa licha ya kuwa na uhakika kwamba mifumo ya mitihani haitoi mwanya wa udanganyifu, wizara imeamua kufanya uhakiki wa kina ili kuthibitisha uhalali wa taarifa hizo.

"Sasa tumekubaliana na katibu mkuu aiandikie TCRA wachukue chuo kile kama sampuli kwa sababu ya tuhuma tulizosoma kwenye gazeti, kwenda kufanya uhakiki wa kimfumo kwa matokeo yote, ambayo yameingizwa kwenye Tehama na kuangalia matokeo yanapoingizwa na kubadilishwa nani anabadilisha," alisema Profesa Mkenda.




*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda*

"Kwa utaratibu, mhadhiri anapomaliza kusahihisha mtihani anaingiza mwenyewe kwenye mfumo, zile karatasi zinapelekwa kwa mtahini wa nje. Huyu anaweza kuwa wa chuo kingine au anayetoka nje ya nchi. Ikitokea yeye ameona kuna haja ya kufanyika mabadiliko, ni lazima yaende kwenye kamati ya mitihani kabla ya kuingizwa kwenye mfumo na mkuu wa idara," aliongeza.

Waziri Mkenda aliongeza kwamba hatua zote hizo zinaacha alama hivyo ni vigumu kwa mtu kufanya mabadiliko yoyote ya alama.

Alisisitiza kwamba vyuo vikuu vinasimamia maadili na weledi, hasa katika eneo la mitihani, na kwamba serikali itaendelea kudhibiti mianya ya udanganyifu kwa kuhakikisha mifumo inakidhi viwango vya juu.

Hivi karibuni katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), watu 17 walikamatwa kwa kuwa na vitambulisho na tiketi za mtihani za kughushi kwa lengo la kuwafanyia wanafunzi halali mitihani yao. Makamu mkuu wa chuo hicho, Profesa Elifas Bisanda, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Habari

# Rais Samia aonya kuhusu SGR



*Rais Samia Suluhu Hassan*

**Na Mwandishi WETU, Dodoma**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa maonyo kadhaa kuhusu uendeshaji wa miundombinu ya reli ya kisasa (SGR) na treni ya mwendokasi inayotumia reli hiyo.

Alitoa maonyo hayo wiki iliyopita jijini Dodoma, wakati akizindua rasmi miundombinu ya reli hiyo na huduma za usafirishaji kupitia reli ya SGR.

Kwanza alilitaka Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Watanzania kwa ujumla, kuhakikisha wanaitunza reli hiyo na kuitumia kwa mujibu wa matakwa yake ili iwe na manufaa kwa nchi na watu wake.

Alisema iwapo reli hiyo haitatunzwa vyema, basi haitakuwa na faida inayotarajiwa.

Rais Samia alizitaka mamlaka kadhaa ikiwamo TRC, wizara mbalimbali na wafanyabiashara kufanya kila juhudi kuambatanisha shughuli za reli hiyo na uwekezaji katika sekta mbalimbali ili kuwa na faida mtambuka.

"Iwapo tutashindwa kuitumia reli hii kwa manufaa, basi tusishangae iwapo itawanufaisha wageni," alisema Rais Samia katika sherehe hizo za uzinduzi zilizofanyika katika kituo cha reli ya kisasa jijini Dodoma kilichopewa jina la Samia.

Rais Samia alisema uwekezaji mkubwa uliofanywa katika Bandari ya Dar es Salaam na maeneo mengine, utakuwa na maana sana iwapo utafungamanishwa na reli hiyo yenye uwezo mkubwa wa kusafirisha shehena nyingi na abiria wengi.

Alisisitiza kuwa shughuli za treni hiyo zifungamanishwe na shughuli nyingine za kiuchumi katika sekta za viwanda, kilimo, madini, bandari kavu na usafirishaji kwa kuzitaja sekta chache.

Kiongozi huyo wa nchi alisema ili kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi na tija kwenye reli ya SGR, Rais Samia aliiagiza TRC kuhakikisha kunakuwa na mifumo miwili ya kifedha itakayotofautisha SGR na reli ya zamani.

Katika hatua nyingine, ili kuhakikisha kuwa TRC inaitumia reli hiyo kwa ufanisi, aliiagiza Ofisi ya Msajili wa Hazina kukaa na bodi na menejimenti ya TRC na kukubaliana malengo mahsusi ya uendeshaji wa reli hiyo.

Alisema malengo hayo ndiyo yatakayotumika kupima mafanikio ya uendeshaji wa SGR.

Lakini akawaleza wafanyakazi wa TRC kuwa malengo hayo mapya hayataweza kufikiwia iwapo hawatabadilisha utamaduni wao wa utendaji kazi.

Alisema treni hiyo na miundombinu yake siyo tu ni mipya, bali inatumia mifumo tofauti na ile waliyoizoea, hivyo kuna umuhimu wa kujenga

Inaendelea Uk. 21



Habari

# Rais Samia aonya kuhusu SGR

Inatoka Uk. 20

utamaduni mpya wa utendaji ili kuviwezesha vitu hivyo kuonyesha tija na ufanisi wake.

**Majina ya vituo**

Wakati huohuo Rais Samia aliridhia ombi la bodi ya TRC kuvipa majina ya viongozi vituo vikubwa vya reli ya SGR.

Katika hafla hiyo, Rais Samia alitangaza kuwa kituo kilichopo katika jengo la Tanzanite jijini Dar es Salaam, kitaitwa Magufuli ili kuenzi uthubutu wake wa kuanza utekelezaji wa mradi huo, wakati kile cha Morogoro kitaitwa Kikwete, ambaye serikali yake ndiyo ilifanya upembuzi yakinifu wa mradi huo.

Alisema kituo cha Dodoma kitaitwa Samia wakati kile cha Mwanza kimepewa jina la Julius Nyerere.

Rais Samia alisema kituo cha Shinyanga kitaitwa Abeid Amani Karume wakati kile cha Tabora kimepewa jina la Ali Hassan Mwinyi na kituo cha Kigoma kitaitwa Benjamin Mkapa, ambaye serikali yake ndio ilikuja na maono ya mradi huo mkubwa.

"Tutaendelea kutoa majina kwa vituo vingine kulingana na mahitaji yatakavyokuwa," alisema.

Pia Rais Samia aliwashukuru wadau mbalimbali kwa kuiunga mkono serikali katika kugharamia ujenzi wa reli hiyo.

Alitoa shukran mahsusi kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kutoa mkopo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande viwili vya reli hiyo.

Pia Rais Samia alilishukuru Shirika la Chakula Ulimwenguni kwa kutoa mabehewa manane kwa ajili ya kuafirisha chakula.

Aidha, Rais Samia alisema kuwa ingawa kazi ya ujenzi wa reli hiyo haujakamilika, serikali imeashaanza harakati za kuimarisha Reli ya Tazara ili kuhakikisha kuwa usafirishaji unaimarishwa katika ukanda ambao reli hiyo inapita.

Awali, Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, aliiambia hadhara kuwa hadi hivi sasa serikali imeshatumia zaidi ya shilingi trilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo ambayo itakapokamilika itakuwa na urefu wa kilometa 2,102 kutoka Dare s Salaam hadi DRC kupitia Burundi.

Tayari ujenzi wa reli yenye urefu wa kilometa zaidi ya 700 kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kilichogawanywa katika mafungu mawili, kimeshakamilika.

Wakandarasi wanaendelea na ujenzi katika vipande vingine kati ya Dodoma na Tabora, Mwanza na Kigoma.

Waziri huyo alisema hadi hivi sasa kazi ya ujenzi inaendelea katika mafungu matano yanayohusisha kilometa 1,560.

"Tunatarajia kuunganisha Tanzania na Burundi kupitia reli hii katika ujenzi wa fungu la saba kutoka Uvinza hadi Msongati kabla haijaendelezwa hadi DRC," alisema.

Wazo la ujenzi wa reli hiyo lilianza wakati wa serikali ya awamu ya tatu chini ya Rais Benjamin Mkapa.

Alipoingia rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete alianza harakati za utekelezaji wa mradi huo ingawa wakati huo mpango ulikuwa ni kujenga reli ya SGR itakayotumia na treni ya kawaida.

Alipoingia Rais John Magufuli, katika awamu ya nne akaamua kuwa reli hiyo ya SGR itumiwe na treni ya umeme na akaanza ujenzi wa mrad huo katikati ya wasiwasi kuwa nchi haitamudu gharama kubwa za mradi huo unaokadiriwa kuhitaji zaidi ya shilingi trilioni 20 hadi utakapokamilika.



*Rais Samia Suluhu Hassan akiwa anaelekea kupanda treni ya SGR kwa ajili ya uzinduzi uliofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam. (Picha na Ikulu)*

Habari

# Hatimaye wakulima wa mahindi Rukwa walipwa



Na Mwandishi WETU,

WIKI moja baada ya Pambazuko kuchapisha malalamiko ya wakulima kutoka Mkoa wa Rukwa, wakidai kutolipwa fedha zao baada ya kuuza mahindi kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), hatimaye wamelipwa.

Wakulima hao walinza kupokea malipo yao Alhamisi iliyopita na hadi kufikia juzi – Jumamosi, karibu wote walikuwa wamepokea fedha zao.

Wiki iliyopita Pambazuko liliwanukuu baadhi ya wakulima hao walilalamika kuwa hawajapokea malipo yao kwa zaidi ya wiki mbili, baada ya kuuza mahindi yao.

"Ni zaidi ya wiki mbili sasa hatujui tutalipwa lini. Tulipowapigia simu viongozi (wa NFRA) wa kanda walisema bado hawajapewa fedha..."

"Rais Samia alipokuja huku Rukwa alituhamasisha kwamba tuuze mahindi yetu NFRA na tumefanya hivyo. Lakini tunashangaa kwa nini tunapigwa danadana malipo yetu," alihoji mkulima mmoja wakati akizungumza na Pambazuko.

Kutokana na malalamiko hayo ya wakulima, Pambazuko liliwatafuta maofisa wa ngazi za juu wa NFRA ambapo walikiri kuchelewa kwa malipo hayo wakisema kumesababishwa na kuchelewa kwa taratibu za kifedha.

Meneja wa NFRA Mkoa wa Rukwa, Marwa Range, alikiri wakulima hao kutolipwa mapema kutokana na utaratibu wa malipo uliowekwa, ambapo mtu anayeuza mahindi anapaswa kulipwa baada ya siku 14.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NFRA wa Kanda, Dkt. Andrew Komba, naye aliliambia Pambazuko kuwa tayari wakulima hao walianza kuingiziwa malipo yao.

"Kwanza utaratibu ni siku 14 kwa sababu lazima mahindi yakaguliwe, yapelekwe maabara na yakikidhi vigezo ndiyo tunaanza kuwalipa wahusika. Sasa wao tangu wameleta mahindi bado haijatimia siku 14," alisema Komba.

Akizungumza na gazeti hili juzi, mmoja wa wakulima hao ambaye hakutaka kutajwa gazetini, alishukuru gazeti la Pambazuko kwa sababu limesaidia "kuskuma" kupatikana kwa malipo ya wakulima hao.

"Tunawashukuru sana kwa kutupazia sauti, hatimaye tumelipwa fedha zetu za mahindi wote tumepata, ninyi Pamabzuko kweli ni chombo cha umma" alisema mkulima huyo.

Kwa kipindi cha wiki nzima, baadhi ya wakulima hao waliendela kumpigia mwandishi wa Pambazuko baada ya kuchapisha habari iliyowahusu wakitaka kujua matokeo ya malalamiko yao.

Juzi walipolipwa waliwasiliana na gazeti la Pambazuko na kushukuru waandishi waliofuatilia habari yao na hatimaye matokeo kupatikana.

Wakati akizindua maghala ya kisasa ya NFRA katika eneo la Kanondo mkoani Rukwa, Julai 16, 2024, Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza wakulima kulipwa shilingi 70,000 kwa gunia la mahindi watakayouza kwa wakala huyo.

Vilevile Rais Samia aliwataka wakulima kutosafirisha mahindi nje ya nchi kwa ajili ya kuuza bila kuwa na vibali kutoka serikalini.

# Mbatia amuonya Samia...

Inatoka Uk. 12

CCM, kwa mfano, ule uchaguzi mkuu wa mwaka 1995, mgombea urais wa NCCR-Mageuzi, Augustine Mrema, sasa marehemu, aliitikisa CCM mpaka Mwalimu Nyerere (Julius) akalazimika kuingilia kati ili kukiokoa chama hicho tawala kisishindwe kwenye uchaguzi huo..."

"Mwaka 2015, mgombea urais wa Ukawa (Umoja wa Katiba ya Wananchi), Edward Lowassa, sasa marehemu, aliitikisa nchi na kusababisha dola yote kuwa hoi bin taaban, kwa sababu nguvu aliyokuwa nayo Lowassa haikuwa ya kawaida..."

"Hata uchaguzi wa mwaka 2020, mgombea urais wa Chadema, Tundu Lissu, alikuwa na nguvu zisizokuwa za kawaida. Wakati wa uchaguzi huo, mgombea urais wa CCM, John Magufuli, alistushwa na mapokezi aliyopata Lissu siku alipokwenda kuhutubia Chato..."

"Yaani Magufuli alijiuliza maswali mengi, kwamba hivi kama wananchi wa Chato wamejitokeza kwa wingi kiasi kile kumpokea Lissu wakati yeye alikuwa amewapelekea miradi mingi, hali itakuwaje kwenye kupiga kura," ameongeza Mbatia.

**Alaumu migogoro**

Akizungumzia hali ya vyama vya siasa nchini, Mbatia ameonyesha kutoridhishwa na mazingira ya vyama hivyo kwa kile alichosema kuwa vinapandikiziwa migogoro na watu wachache wasiotaka maendeleo ya vyama hivyo.

Mbatia alitoa mfano Chama cha NCCR-Mageuzi kilivyokuwa maarufu katika miaka ya 1995 kisha kikadhoofika baada ya kuwa na migogoro ya uongozi na kisha Chama cha Wananchi (CUF) ambacho nacho kilidhoofishwa na migogoro baada ya kuwa maarufu katika miaka ya 2000 hadi 2005.

"Hata Chadema ambacho kwa sasa ndicho chama kikuu cha upinzani, mnaona jinsi kinavyotikishwa na migogoro ambayo haileti picha nzuri kisiasa..."

"Tatizo letu kubwa ni kwamba hatuko salama kama nchi kwa sababu hatuna mifumo imara na endelevu kiutawala..."

"Pia, hapa nchini kwetu kuna baadhi ya watu wanajiona wao ni bora kuliko wengine, ndiyo maana hawataki mabadiliko hata ya kikatiba, licha ya serikali kuunda baadhi ya tume zilizokuja na mapendekezo mbalimbali zikiwamo Tume ya Nyalali ya mwaka 1998 pamoja na Tume ya Warioba ya miaka ya hivi karibuni.."

.

"Kwa ufupi tu ni kwamba, nchi yetu tuko katika mfumo wa vyama vingi kwenye mfumo wa CCM na ushahidi wa hilo ni pale ambapo mkuu wa wilaya ambaye ni kiongozi wa serikali, anakuwa mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya CCM," amesema.

Kuhusu migogoro ya kisiasa iliyosababisha aondolewe madarakani NCCR-Mageuzi, amesema imemfanya aimarike zaidi kwa kuwa uwepo wake nje ya chama hicho umemfanya awe na maarifa mengi zaidi.

## Je wajua



**Eneo la Cameron Park lililopo California, Marekani wakazi wake wengi wanamiliki ndege kuliko magari na wameweka maegesho ya ndege hizo pembeni mwa nyumba zao. Mtaa huo ulijengwa 1963 na una nyumba 100.**



**Graça Machel ndiye mwanamke pekee duniani aliyewahi kuwa "first lady" wa nchi mbili tofauti, ni mjane wa aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Nelson Mandela na Samora Machel wa Msumbiji.**

## Mtoto wa Mvuvi



Na Maregesi PAUL

# Hawa ngedere, bundi wadhibitiwe haraka

JULAI 31, mwaka huu, ni siku ambayo mamilioni ya Watanzania hawataisahau.

Kwa wale waliosahau, ni kwamba siku hiyo Shirika la Reli Tanzania (TRC), lilitoa taarifa ya kuomba radhi abiria wake na Watanzania kufuatia hitilafu ya umeme iliyojitokeza katika reli ya kisasa (SGR), kati ya Stesheni za Kilosa na Kidete, mkoani Morogoro na kusababisha treni kuzima ikiwa njiani, baada ya umeme kukatika.

Katika taarifa yake, TRC ilieleza kuwa umeme huo ulikatika kutokana na mnyama wa porini; ngedere na au ndege aina bundi ndiyo waliosababisha hitilafu hiyo.

Taarifa hiyo iliyosainiwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa TRC, Jamila Mbarouk, ilisema ngedere na au bundi, huweza kusababisha hitilafu za aina hiyo pindi wanapogusa nyaya za umeme zilizotandazwa juu ya reli.

Kwa kifupi, taarifa hiyo ilishangaza na kushtua wengi kwa sababu kabla treni hiyo haijaanza safari, TRC walisema vichwa vya treni hiyo vina uwezo wa kufua umeme pindi inapotokea hitilafu ya umeme katika kituo cha kufua umeme.

Aidha, ilielezwa pia kuwa vichwa vingine vina uwezo wa kutumia umeme na dizeli kama mbadala, iwapo kutakuwa na tatizo kwenye mfumo wa umeme.

Kutokana na kusimama kwa safari, inawezekana kabisa kuwa vichwa vya treni tulivyoelezwa kuwa vinaweza kujiendesha kwa muda hata bila umeme wa Tanesco, ilikuwa ni siasa.

Endapo vichwa hivyo vya treni vingekuwa na uwezo huo ulioelezwa awali, ni dhahiri kuwa abiria hao wasingesubirishwa kusubiri umeme uwake kwa muda mrefu.

Kutokana na funzo kutoka kwa ngedere na au bundi, sasa ni wajibu wa TRC kutumia njia zote kudhibiti viumbe hao kwa sababu usafiri wa SGR utaonekana hauna maana ikiwa viumbe hao wanaweza kuusimamisha.

Kwa kuwa serikali imetumia matrilioni ya fedha kuanzisha usafiri huo nchini na kuweka miundombinu ya kudhibiti binadamu ambao wana akili na maarifa ya kufanya uharibifu wa aina mbalimbali, haiwezi kushindwa kufanya uwekezaji mwingine kwa ajili ya kudhibiti viumbe wengine wanaoweza kuleta madhara katika mradi huo muhimu wa kimkakati.

Ngedere na wanyama wasiachwe kuwa na uhuru wa kukanyaga nyaya za umeme na kuathiri uendeshaji wa treni hiyo ambayo mamilioni ya Watanzania wanaamini itakuwa ni mkombozi wa usafiri wa nchi kavu nchini.

Aidha, bundi na aina nyingine ya ndege lazima wadhibitiwe ili wasilete madhara na hasara kubwa kwa Tanzania.

Kama viumbe waharibifu wa aina ya ngedere na au bundi hawatadhibitiwa mapema, heshima, umuhimu na umaarufu wa SGR utashuka na hivyo kuwafanya abiria waogope kuutumia usafiri huo.



## Habri katika picha



*Mpita njia akingalia rundo la taka lilizotapakaa hadi nje ya jengo la kutunzia taka hizo lililopo karibu na migahawa ya chakula katika eneo Stendi ya Daladala Makubusho kutokana na Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, kushindwa kuziondoa kwa wakati, (Picha na Fidelis FELIX)*



*Kiongozi mstaafu wa chama cha ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, akizungumza kwenye mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika katika Kata ya Ugalla iliyopo Jimbo la Nsimbo mkoani Katavi juzi. (Picha ACT-Wazalendo)*



*Beki wa Yanga, Nickson Kibabage akimtoka mchezaji wa Red Arrows ya Zambia katika mechi ya kirafiki iliyochezwa uwanja wa Mkapa jana. Yanga iliibuka na ushindi wa magoli 2-1. (Picha na Yanga)*

*Mkuu wa Utawala na Rasilimali Watu wa Kampuni ya Bima ya Strategis ya Tanzania, Joyce Kulwah Mison akifurahi kutimiza miaka 50 katika hafla fupi ya kumpongeza iliyofanyika Masaki, Dar es Salaam wiki iliyopita. (Picha na Brown24).*



Kenya



*Raila Odinga*

# Ruto 'ararua' upinzani, ODM yaweweseka

Na Julius MKAMBI, Nairobi

MAANDAMANO ya vijana wa GenZ nchini Kenya yamegeuka faida kubwa kisiasa kwa Rais William Ruto na kuwa mwiba kwa muungano wa vyama vya upinzani chini ya mwamvuli wa Azimio la Umoja.

GenZ 'walimshika mateka' Rais Ruto kutokana na maandamano yaliyokuwa yanafanyika nchi nzima wakishinikiza serikali kuwajibika, harakati ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zikifanywa na upinzani wakiongozwa na Raila Odinga.

Miongoni mwa masharti ya GenZ waliyotaka Rais Ruto kutekeleza ni kuvunja baraza la mawaziri, jambo ambalo alilifanya lakini alipotangaza awamu ya kwanza ya baraza jipya lililokuwa na mawaziri wateule 11, Ruto aliwarudisha kazini mawaziri sita kati ya wale 'aliowatema.'

Hatua hiyo iliwakasirisha tena GenZ na viongozi wa upinzani, lakini Rais Ruto alipodokeza baraza la mawaziri jipya litakuwa pana kwa kujumuisha upinzani, lugha ya Azimio la Umoja ilikua moja tu; hawatakubali kujiunga na serikali inayoongozwa na Kenya Kwanza.

Rais Ruto alihimiza mazungumzo ya kitaifa kupata suluhu ya hoja zilizoibuliwa na GenZ, kauli ambayo iliungwa mkono na Raila na kuibua tetesi awamu ya pili ya mawaziri itajumuisha baadhi ya wanachama wa Orange Democratic Movement (ODM) inayoongozwa na Raila.

Raila amekuwa akihitaji zaidi kuungwa mkono na Ruto katika harakati zake za kuwania uenyekiti wa Tume Umoja wa Afrika (AU).

Ruto alitimiza ahadi yake kuunda serikali pana alipowajumuisha viongozi wanne waandamizi wa ODM ambao ni mwenyekiti John Badi, kiongozi wa wengi Bunge la Taifa, Opiyo Wandayi na manaibu viongozi Wycliffe Oparanya na Hassan Ali Joho.

Naye kiongozi wa chama cha Wiper, ambacho ni moja ya vyama vinavyounda Azimio la Umoja, Kalonzo Musyoka, alikataa 'ofa' aliyopewa na Rais Ruto kuwa Mkuu wa Sheria akisisitiza hayupo tayari kujiunga na serikali.

Kalonzo alisema kuwa kufanya hivyo itakuwa ni kuwasaliti GenZ ambao baadhi yao wapo waliopoteza maisha, kurejuhiwa, kutupwa rumande na hata wengine kutekwa, wakishinikiza serikali kuwajibika.

Hata hivyo, baadhi ya wanachama wa ODM waliridhika na uteuzi uliofanywa na Rais Ruto, huku wakiwaomba vijana wa GenZ kusitisha maandamano na kumpa rais muda wa kutekeleza majukumu.

Ni dhahiri misimamo tofauti ya viongozi wa ODM umegawa umoja kiasi cha kuonekana sasa upinzani unadhoofika.

Kutokana na mitazamo tofauti, Muungano wa Azimio la Umoja unazidi kumeguka, hususan sasa baada ya Rais Ruto kujumuisha upinzani katika serikali.

Tayari kuna shinikizo kutoka vyama vya Azimio kumtaka aliyekuwa Makamu Rais, Kalonzo Musyoka, kushika nafasi ya kiongozi mpya wa Azimio la Umoja kwa kuwa madai ODM 'imemezwa' na Ruto. Kwamba hawamtaki Raila.

Aidha, wapo viongzozi wanaotaka vyama kujiondoa katika umoja huo na kuunda muungano mpya na kuiacha ODM pekee yake.

# Wazazi wabuni mbinu kulinda watoto

Na Hellen NGOROMERA

WAZAZI katika baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam, wamechukua hatua kuhakikisha usalama wa watoto ikiwa ni njia kukabiliana na wimbi la utekaji na mauaji dhidi yao.

Pambazuko limebaini kuwa katika mitaa mbalimbali, wazazi wengi wameanzisha utaratibu wa kuhakikisha watoto wao wanasindikizwa na watu wanaowaamini wakati wa kwenda shule na kurudi nyumbani.

Hali hiyo imechochewa na kuendelea kwa matukio ya utekaji wa watoto, hasa wanaosoma shule za msingi.

Kufuatia wimbi la watoto kudaiwa kutekwa, tayari Jeshi la Polisi limekamata watu kadhaa wakihusishwa na matukio hayo.

Watu hao walikamatwa kutokana na jitihada za wananchi wenyewe wakishirikiana na vyombo vya dola.

Pambazuko limebaini kuwa katika shule kadhaa jijini Dar es Salaam asilimia kubwa ya watoto wanapelekwa na kufuatwa shule na wasindikizaji, wakiwamo wazazi na walezi.

Mariamu Rashid, mkazi wa Mtoni Kijichi ameliambia Pambazuko kwamba ameamua kumpeleka shuleni na kumfuata mtoto wake anayesoma Shule ya Msingi Kijichi ili kumwekea ulinzi kutokana na kukithiri kwa matukio ya utekaji wa watoto.

Beatrice Mkombwa, ambaye mtoto wake anasoma Shule ya Msingi Mtoni Mtongani, anasema hivi sasa analazimika kumpeleka mtoto wake shuleni na baadaye kumfuata akishamaliza masomo.

“Hali ni mbaya ndugu mwandishi, wimbi hili la utekaji watoto linatuweka katika hofu kubwa. Tunaliomba Jeshi la Polisi liiangalie hali hii ili kuwaweka watoto salama,” amesema Damian Mkufya, mkazi wa Kijitonyama.

Katika nyumba za ibada pia viongozi wake wamekuwa wakitoa tahadhari kwa waumini wao kuhusu hali hiyo na kuwasihi wazazi kuchukua hatua ya kulinda watoto wao.

Wiki iliyopita katika Kanisa Katoliki Epifania – Kijichi, Katibu wa rarokia hiyo, Rose Soloka, aliwasihi waumini kuchukua tahadhari kwa kuwawekea ulinzi watoto wao.

Kijichi na Mbagala ni miongoni mwa maeneo ambayo yameathirika zaidi na matukio ya utekaji na kuuawa kwa watoto.

Hali kadhalika kanisa hilo limebadili ratiba ya mafundisho kwa watoto wanaotarajiwa kupokea sakramenti za Ekaristi Takatifu na Kipaimara ili kuwaepusha na vitendo hivyo.

Ratiba mpya ya mafundusho hayo ilitangazwa wiki iliyopita na katikesta mkuu wa parokia hiyo, Isdory Anslemo.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda, aliliambia Pambazuko hivi karibuni kwamba kutokana na hali hiyo kwa kushirikiana na wadau, ofisi yake imeanza kutoa elimu katika shule za manispaa hiyo ili kudhibiti vitendo hivyo.

**Diwani naye ajiunga**

Diwani wa Kata ya Makurumla, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Bakari Kimwanga, naye ameanzisha kampeni maalum katika kata yake kuhamasisha wazazi na watu wengine kuweka mikakati ya kuwalinda watoto dhidi ya watekaji.



*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima.*

Fikra Mujarab

# Ndani ya mipaka ya uhuru wa habari kuna nongwa!



*Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa*

Na Peter NYANJE

"HAKUNA uhuru usio na mipaka," ni kauli ambayo tumezoea kuiskia aghalabu kutoka kwa viongozi wa serikali pale wanapokemea waandishi wa habari.

Siyo hao pekee, bali pia kauli hiyo hugusa vyombo vya habari na wanaharakati pale wanapotumia njia anuai za mawasiliano kufikisha ujumbe kwa jamii.

Ni moja ya kauli ambazo zimetolewa na viongozi mara nyingi, kiasi kuwa sasa imeanza kuzoeleka masikioni mwa wengi.

Hivi karibuni, tumemsikia Rais Samia Suluhu Hassan akiirudia kauli hii katika hotuba yake baada ya kuwaapisha viongozi kadhaa aliowateua.

Alikuwa anatoa maelekezo kwa waziri mpya wa habari, mawasiliano na teknolojia ya habari, Jerry Silaa, kuwa anapokwenda kuifanya kazi zake, ahakikishe kuwa vyombo vya habari vinazingatia kuwa hakuna uhuru usio na mipaka.

Wala sina tatizo na kauli hiyo kwa sababu ina ukweli mwingi ndani yake.

Kweli haipendezi pale mtu anapovuka mipaka ya uhuru aliokuwa nao kwa sababu kufanya hivyo kunamaanisha kuwa unaingilia maslahi ya mtu mwingine.

Hilo ni jambo lisilofaa, na ndio maana wala sioni shida mtu anapoadhibiwa kwa kufanya mambo yaliyo nje ya uhuru wake.

Shida yangu ni kutozingatiwa kwa haki ambazo mtu anazo ndani ya uhuru ambao hutolewa kisheria.

Wakati viongozi wetu wakitukumbusha kuwa uhuru wetu una mipaka, na wao wanapaswa kukumbuka kuwa ndani ya mipaka hiyo, tuna uhuru na wao wana wajibu wa kuhakikisha hakuna kinachokwaza sisi kuutumia uhuru wetu ndani ya mipaka iliyowekwa kisheria.

Watuadhibu tunapiovuka mipaka, lakini wasifanye hivyo tutakapotekeleza haki zetu zilizopo ndani ya mipaka ya uhuru tuliopewa kisheria.

Kinachosikitisha ni kuwa mara nyingi tumeshuhudia uhuru huo ukibanangwa na hakuna 'fidia' ya maana kwa wale ambao uhuru wao umeminywa kinyume cha sheria.

Nitoe mifano kadhaa; kwanza, kwa mujibu wa sheria za habari, vyombo vya habari na hata watu binafsi, sasa wana haki ya kupata taarifa kutoka ofisi zote za umma.

Upo utaratibu uliowekwa kisheria kwa mtu anayetaka taarifa kutoka katika ofisi ya umma.

Lakini inashangaza kuwa hata baada ya kufuata utaratibu uliowekwa kisheria, bado watu wanakosa taarifa hizo au wanazipata kwa kuchelewa sana.

Inaendelea Uk. 29



*Waandishi wa habari wakiwa katika majukumu yao. (Picha na Mtandao)*

# Ndani ya mipaka ya uhuru wa habari kuna nongwa!

Inatoka Uk. 28

Ni jambo la kushangaza kuwa sheria inaelekeza wananchi wapatiwe taarifa kutoka ofisi za umma ndani ya muda Fulani, lakini maofisa katika ofisi hizo wanakiuka sheria hiyo kwa kuzuia utoaji wa taarifa hizo au kuzitoa kwa kuchelewa.

Kupatiwa taarifa hizi ni jambo ambalo lipo ndani ya uhuru uliowekwa kupitia sheria ambayo serikali yenyewe imeitunga.

Kwa nini sheria hiyo inapokiukwa na walioitunga hakuna hatua zinazochukuliwa?

Sidhani kama vyombo vya habari au waandishi wa habari wanavuka mipaka yao wanapokwenda kuomba taarifa kwenye ofisi za umma.

Lakini wanakosa taarifa hizo na hatujawahi kusikia mtu akiadhibiwa kutokana na kukiuka sheria hiyo.

Lakini mwandishi au chombo kikivuka kidogo tu mipaka ya uhuru wake, tumekuwa tukishuhudia hatua zikichukuliwa na "mikono mirefu ya serikali."

Mfano mwingine unahusu hukumu zilizowahi kutolewa na mahakama, zikivipa vyombo vya habari ushindi dhidi ya sheria kandamizi ambazo serikali ilizitunga.

Moja ya kesi maarufu inayofahamika ni ile iliyofunguliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na wadau wengine kwenye mahakama ya Afrika Mashariki (EACJ) miaka kadhaa iliyopita.

Katika kesi hiyo, wadau hao wa habari walikuwa wanapinga vifungu kadhaa vya sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari na mahakama ikakubaliana nao na kusema kuwa vifungu vingi katika sheria hiyo vinakiuka haki ya kupata habari iliyopo kikatiba, jambo ambalo ni kinyume pia na mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mahakama ikaamuru vifungu hivyo aidha virekebishwe au viondolewe kabisa.

Lakini hadi hii leo serikali imefanya marekebisho kwenye vifungu vichache tu kati ya vile ambavyo EACJ ilisema vinakiuka uhuru wa habari.

Mahakama iliamuru hivyo baada ya kubainisha kuwa sheria hiyo ina vifungu vingi ambavyo haviendani na haki ya kupata habari chini ya Katiba.

Kupitia sheria ambazo serikali imezitunga, vyombo vya habari nchini vina uhuru wa kutafuta, kukusanya, kuchakata na kusambaza habari.

Lakini sheria hizohizo bado zina vifungu ambavyo vinatoa mamlaka kwa maofisa wa serikali kuamua ni kipi kinapaswa kuchapishwa na vyombo vya habari – rejea Kifungu cha 7 (2) (a) (v) cha sheria ya huduma za vyombo vya habari.

Jambo la kusikitisha ni kuwa wakati kifungi cha 7(1) kinatoa haki kwa vyombo vya habari kutafuta, kukusanya, kuchakata na kusambaza habari, kifungu kidogo cha pili kinaweka masharti lukuki kuhusiana na utekelezaji wa haki na wajibu huo, kiasi kuwa ukichambua kiundani ni kama kinaweka pingamizi kwa haki zote ambazo zimetolewa kwenye kifungu cha 7(1)!

Wakati serikali ikihakikisha vyombo vya habari havivuki mipaka ilivyowekewa, nadhani wakati umefika sasa kwa serikali pia kuhakikisha kuwa hakuna vikwazo kwa vyombo vya habari kutekeleza majukumu yake yaliyomo ndani ya uhuru waliopatiwa kisheria.

Sudan

# Hofu ya njaa kali yatanda Darfur

**Darfur, Sudan**

KAMBI kubwa ya wakimbizi iliyoko eneo la Zamzam, huko Darfur, huenda ikalipuka kwa magonjwa kufuatia kuwepo dalili za njaa kali.

Watu zaidi ya 400, 000 wanaohifadhiwa ndani ya kambi hiyo, wengi wao wakiwa wanawake na watoto, huenda wakatingwa na magonjwa yanayoambatana na njaa ama vifo, ikiwa hawatapata msaada wa haraka.

Umoja wa Mataifa (UN), kupitia kamati yake ya kukagua kiwango cha njaa, imethibitisha pasipo na shaka, kiwango kikubwa cha njaa katika kambi hiyo, iliyo karibu na mji wa El Fasher, ndani ya jimbo la Darfur.

Vita vilivyodumu kwa miezi 15 ndani ya nchi hiyo, vimesababisha madhara kadhaa yakiwemo uhamaji wa watu na njaa kubwa, inayowakumba watu wengi waishio maeneo ya Darfur Kaskazini mwa Sudan.

"Tunahitaji kwa haraka upanuzi mkubwa wa upatikanaji wa misaada ya kibinadamu ili tuweze kukomesha njaa katika eneo la Darfur Kaskazini na kukomesha kuenea kote Sudan," Mkurugenzi Mtendaji wa Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Cindy McCain alisema.

Tangu Aprili 2023, nchi hiyo imeshuhudia vita kati ya Jeshi la Serikali ya Sudan na kikundi cha Rapid Support Forces(RSF).


" Pande zinazopigana lazima ziondoe vikwazo vyote na kufungua njia mpya za usambazaji wa vyakula mipakani, na katika maeneo ya migogoro, ili mashirika ya misaada yaweze kufika kwa jamii zilizo katika hali mbaya na chakula na misaada mingine ya kibinadamu inayohitajika," aliongeza McCain.

UN imesema kuwa tangazo la njaa katika eneo hilo linathibitisha hofu ya jumuia ya kibinadamu na linafuata uchambuzi wa mwezi Juni unaoonyesha kupungua kwa kiasi kikubwa kwa usalama wa chakula na lishe, huku watu 755,000 wakikabiliwa na hali mbaya.

" Kama misaada ya dharura haiwezi kuwasilishwa kwa jamii zilizokwama katika maeneo yenye migogoro kama vile Darfur, Khartoum, Kordofan na Al Jazirah. Hali bado ni mbaya nchini kote, huku takriban watoto 730,000 wakitarajiwa kukumbwa na utapiamlo mkali mwaka huu," imeongeza UN.

***Chanzo: TRT- Africa***

## Mshindi wetu ni Don Mselle




***Pambazuko limepokea tafsiri 473 kutoka kwa wasomaji wake, na baada ya kuzipitia, zimepatikana bora zaidi tatu kutoka kwa; Don Mselle, Masaga na Greenland Investment. Aliyeibuka kinara ni Don Mselle ambaye anapokea Shilingi 10,000. Tafsiri ya Don ni hii; Wakati dunia imetumbukia kwenye teknolojia ya simu na kompyuta, roboti nazo zimerejea kwenye kusoma na kupata maarifa kwenye michoro na vitabu vilivyoachwa na binadamu. Pambazuko linawapongeza wote walioshiriki na kuwaomba waendelee kusoma gazeti na kuchemsha bongo kupitia ukurasa wa 5 - Mhariri***



Na Hellen NGOROMERA





# Tamu, chungu ya ndugu wa tumbo moja kuolewa na mume mmoja - 2

Habari za leo ndugu msomaji wa safu ya uhusiano.

Wiki iliyopita nilijadili kuhusu ndoa za ndugu zinavyoweza kusababisha uimara ndani ya familia.

Lakini mwishoni mwa makala hiyo, nikadokeza kuwa kwa upande mwingine, ndoa za aina hiyo zinaweza kuwa sababu ya kudhoofisha na hata kusambaratisha familia. Sasa tuendelee.

Wakati kuna shuhuda kuonyesha kuwa ndoa zinazohusisha wake wawili ambao ni wa kuzaliwa na mama mmoja mambo yanakuwa mazuri, hasa kwenye suala la malezi na matunzo ya watoto, lakini pia kwa upande mwingine, kuna visa ambavyo vinaonyesha kuwepo kwa shida.

Utaratibu huu huzua mitafaruku hasa pale inapotokea mdogo mtu anakuwa na tamaa ya kutaka kumpindua kabisa dada yake ili yeye abake mke pekee.

Nimewahi kushuhudia kisa kimoja; mwanaume alikuwa akiishi na mkewe na watoto, kisha baadaye shemeji yake, yaani mdogo wa mke wake, akaungana nao na kuishi pamoja.

Baada ya kuishi kwa miaka kadhaa, yule shemeji akaamua kurudi kijijini kwa wazazi wake, lakini cha ajabu baada ya muda, mwanamume yule alienda kijijini ambako baada ya kupata ridhaa ya wazazi, akamuoa shemeji yake.

Kumbe wakati wanaishi pamoja mjini, alikuwa anatembea naye kwa siri.

Kitendo cha wawili hao kuoana, kilimshitua dada mkubwa ambaye hatimaye alibaini kuwa ndugu yake alikuwa akimzunguka kwa mume wake.

Hapo mtafaruku mkubwa ulizuka baina ya ndugu hao wawili na hakukuwa na maelewano kati yao tena.

Jambo hilo lilisababisha pia hata watoto wa ndugu hao walioolewa na mume mmoja kutoelewana kabisa (maana yule mwanamume alizaa pia na mdogo mtu baada ya kumuoa)!

Nini chanzo cha mwanaume kuamua kuoa mwanamke zaidi ya mmoja? Moja kati ya mambo yanayosababisha hivyo ni mila katika baadhi ya makabila nchini ambazo zinaruhusu jambo hilo.

Mila hizo zinaruhusu jambo hilo zikiamini kuwa ndugu wa tumbo moja anayeolewa na mume wa dada yake atakuwa mlezi mzuri wa watoto wa endapo dada yale atafariki kabla yake.

Lakini, je, ni sahihi mwanaume kuoa ndugu wa damu wa mkewe?

Ikiwa mume anahitaji kuongeza mke, ana wajibu wa kumweleza mkewe ndipo aridhie kufanya hivyo au?

Binafsi sioni sababu ya mwanaume kuamua kujichukulia mamlaka ya kuoa mke mwingine, tena bila sababu za msingi ikiwa mke hataridhia!

Ikiwa itatokea ulazima wa kufanya hivyo, bora mwanaume aoe mwanamke mwingine tofauti na ndugu yake wa damu Tukutane wiki ijayo.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0754 88 67 49.***

Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

# Mbinu za kupendeza bila gharama kubwa

WATU wengi huona kuwa kununua nguo ya gharama kubwa ama kutumia pesa nyingi kushona nguo, ndiyo huwafanya kupendeza, jambo ambalo siyo kweli.

Suala la kupendeza ni namna unavyoweza kupangilia mavazi yako kwa mfuatano wa rangi husika.

Leo katika safu hii nitagusia kuhusu rangi nyeusi na nyeupe na namna ambavyo zitampa mtu muonekano mzuri na wenye kuvutia.

Gauni ya rangi nyeupe unaweza kulivaa na koti la rangi nyeusi, pinki ama kijani, na ukapata mwonekano wa gharama hata kama umenunua nguo za bei rahisi.



Gauni la rangi nyeusi unaweza kulivaa na koti la rangi nyeupe, bluu 'laini' au pinki.

Katika mavazi haya, vaa viatu virefu vya rangi nyeusi vya kufunika vinaendana zaidi na pia, kwa mwanamke ni vyema kubeba pochi ya rangi nyeusi ili kukamilisha vazi lenye muonekanano wa kuvutia.

Vazi hili unaweza kulivaa ofisini na likakupa muonekano wa gharama kubwa.

# Unavyoweza kurefusha kope zako

KOPE ni moja ya sehemu muhimu katika sura ya binadamu (siyo mwanamke pekee), ambapo pamoja na sababu za kisayansi kuwepo, kuna zile za kiurembo pia.

Kope hupendeza zaidi zikiwa ndefu, hivyo huwalazimu baadhi ya wanawake ama wasichana kuzichana kwa 'mascara' ili kuziweka katika hali ya kunyooka na kuvutia, huku wengine wakibandika za bandia.

Pamoja na mbinu hiyo, leo nimekuandalia namna bora ya kurefusha kope pasipo madhara.

Mbinu hiyo ni kutumia mafuta ya mgando ya Vaseline.

Katika kukuza na kujaza kope, paka Vaseline kwenye kope zako kila siku usiku kabla ya kulala. Kwenye zoezi hilo, utaona mabadiliko baada ya wiki mbili hadi tatu.



Afcon




# Waiteni nao wataitika Pamoja Afcon 2027

Na John MARWA

“NAMI nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa”. Ni miongoni mwa maneno matakatifu kutoka katika Kitabu cha Mungu; Biblia kwa Dini za Kikristo (Luka 11:9-10).

Maneno ambayo Mwenyezi Mungu aliwaambia wana wa Israel kuwa kwa kuomba nao watapewa, kwa kutafuta nao wataona na hata wakibisha, basi nao watafunguliwa.

Sasa soka limeombwa kuja Afrika Mashariki, muda ukatafutwa nao ukapatikana na funguo tukakabidhiwa uenyeji wa Pamoja Afcon 2027.

Tanzania, Kenya na Uganda ziko mbioni kuhakikisha zinaandika historia ya kuandaa mashindano ya Mataifa ya Afrika; “Pamoja Afcon 2027,” ambapo maandalizi yamepamba moto kila nchi ikiwa katika maandalizi ya kufanikisha mashindano hayo makubwa Afrika.

Miongoni mwa vitu ambavyo vimeifanya Afrika Mashariki kushinda tiketi hii, ni maendeleo makubwa ya soka katika ukanda huu na namna ambavyo Tanzania imekuwa kitovu kipya cha ushabiki wa soka duniani.

Mashabiki wa soka katika ardhi ya Mwalimu Julius Nyerere, wanaifanya dunia kuitazama Bendera ya Tanzania kwa jicho pevu na ang’avu, na pia ni vigumu kuwataja Watanzania bila kuwapa heshima mashabiki wa Simba na Yanga.

Hawa ndio wanaifanya Afrika inachizika kisoka, inasimama tenge kuitazama Tanzania kwa kutaka kufahamu nini kinaendelea.

Hivi sasa siyo hadithi za Abunwasi, juzi na jana Afrika Masharikia na Afrika yote ilisimama kwa matamasha makubwa mawili; ‘Simba Day’ na ‘Mwananchi Day’.

Si tumeona mzuka wa soka la kulevya ulivyowalewesha tepwele-tepwele wanazi wa soka? Hii inapaswa kuwa ‘trela’ ya kuelekea Pamoja Afcon 2027.

Huu ndio mtaji wa kuwafanya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) wasijutie mlango walioingia kuleta shindano kubwa kuliko yote Afrika.

Acha niwang’ate sikio walevi wa Soka la Tanzania; waambukizine na majirani zenu, wanong’onezeni jinsi ya kupata njaa ya mahaba ya kweli na gozi la ng’ombe, namna ya kuvijaza viwanja kama mnavyofanya nyie.

Na hapa ndipo kamati ya maandalizi inapaswa kuzitumia Simba na Yanga kwa maana ya mashabiki wao kama ‘making scheme’ ya kuifanya Afcon kunoga, maana shughuli ni watu na watu wapo ila unawaletaje kwenye shughuli? Basi wape wenye shughuli zao.

Kama Afrika Mashariki tunaweza kuifanya Pamoja Afcon ikawa mfano wa Afcon zote zilizopita kwa kuhakikisha tunajaza viwanja vyote katika kila mchezo, ni mkakati na mpango tu wa kulitimiza hilo.

Wenzetu wa Kenya na Uganda wako tayari muda wowote, ili kuifanya Afcon kuwa bora zaidi, ndiyo maana tunasema; tukiwaita, wataitika, tukiwaomba waje, watakuja na tukibisha malango ya viwanja vyote, nao watavijaza ila mkakati wa kuwafanya waitike, waje na waingie ndio itakuwa silaha ya ushindi.



# Beyonce: Mrembo anayewachanganya mastaa kibao

**NEW YORK, MAREKANI**

MWANAMUZIKI Beyonce Knowles 'Beyonce au Queen B' ni msanii mwenye kipaji kikubwa cha uimbaji ambaye anatengeneza mkwanja mrefu kupitia kipaji chake.

Ukiondoa kipaji Queen B ni miongoni mwa wanamuziki wanaovutia duniani kwa uzuri, pasina shaka wanaume wengi wanatamani wangekuwa na uhusiano naye au kumuoa kama alivyofanya Jay Z.

Katika maisha yake msanii huyo huwashangaza wengi hasa anapohojiwa kuhusu mahusiano yake huwa anasisitiza kuwa mwanaume wake wa kwanza aliyemtoa usichana ni rapa Jay Z.

Hiyo yote ni kutokana na Beyonce kuwa na historia ya kuwa na uhusiano na wanaume wengine hapo awali.

Hii hapa list ya watu saba waliojaribu na waliowahi kuwa na mahusiano ya wazi na ya siri na Beyonce kabla ya kuwa na Jay Z.

1. Lyndell Locke:, huyu jamaa ndiyo alikuwa mpenzi wa kwanza wa Beyonce kipindi anasoma, unaambiwa jamaa alikuwa akimsindikiza Beyonce kwenye mazoezi ya kuimba na kucheza akiwa kwenye harakati za kujitafuta.

Beyonce anasisitiza kwamba hajawahi kuwa na uhusiano wa chumbani na huyu jamaa.

2. Cam'Ron, aliyewahi kutamba na ngoma yake ya 'Oh Boy'. inasemekana kwamba jamaa huyu alifanya ngoma moja na Beyonce, kisha mwanadada huyo alimpa ofa ya kulala naye chumba kimoja lakini mwanadada huyo anasema hawakufanya kitu chochote, jambo ambalo kila mtu huwa haamini.

3. Justin Timberlake:, Mwanamuziki Justin Timberlake ambaye pia ni rafiki mkubwa wa Jay Z inadaiwa amepata kupiga maraha usiku mmoja na baadaye kufanya vitu vingi. Japokuwa hii habari haikuwa na uthibitisho wowote lakini ilivuma kwa wakati wake.

4. Michael Jackson: Mfalme wa Pop duniani hayati Michael Jackson baada ya msanii huyo kufariki P. Diddy alitoa stori kwamba kuna siku alitaka kwenda kwenye sherehe pamoja na Diddy akiwa na lengo kubwa la kutaka kukutana na Beyonce na kumuelezea hisia zake. Alimuelezea kuwa kumbe Michael Jackson sio mkali wa kuchagua mitindo ya kucheza na midundo tu, hadi wanawake wazuri anajua kuchagua.

5. Mos Def: Huyu ni Mtarishaji wa muziki kutoka katika studio za Def Jam rekodi naye pia, alijaribu kumpata Beyonce akitumia mwanya wa wakati anafanya naye kazi kwa ajili ya MTV, lakini juhudi zake ziligonga mwamba.

6. Sean Paul: Msanii wa ragga na dansi Hall kutoka nchini Jamaica Huyu jamaa ndiyo anasadikiwa kuwa na mahusiano ya siri na Beyonce. Kuna muda walikuwa karibu na kufanya mambo mengi pamoja hadi baadaye kutengeneza ngoma ya 'Baby Boy' ya Beyonce.

Ukaribu huo upo na unaweza kuona kwamba hadi marafiki wa Beyonce ni marafiki wa Sean Paul, kwa mfano mtu kama Kerry Rowland ambaye ameipendezesha ngoma ya 'how deep' ya Sean Paul. Lakini Sean Paul mwenyewe aliwahi kuulizwa kuhusu hii ishu na alikataa katakata.

7. Marquise Huston: Mchizi ni mwigizaji na mwimbaji inadaiwa naye pia aliwahi kutoka kimapenzi na Queen B, Jamaa aliwahi kushikilia bango kwamba aliwahi kuwa na uhusiano na Beyonce akiwa na miaka 17.





## Olmo

Wakala wa kiungo mshambuliaji wa timu ya RB Leipzig, Daniel Olmo ameanza mazungumzo na klabu hiyo kwa lengo la kufanya uhamisho wa mchezaji wake kwenda Barcelona.


## de Ligt



Beki wa kati kutoka klabu ya Bayern Munich, Matthijs de Ligt amezigomea ofa zote isipokuwa ya Manchester United tu tangu mwezi Juni mwaka huu, makubaliano binafsi kati ya mchezaji na Manchester United yamefikiwa.

## Gallagher

Klabu ya Atlético Madrid ipo mbioni kunasa saini ya kiungo, Conor Gallagher kutokea klabu ya Chelsea.



# Tanzania 'yachechemea' Olimpiki 2024 Ufaransa

**Na Mwandishi WETU**

MATUMAINI ya Tanzania kupata medali katika michezo ya Olimpiki 2024, inayoendelea nchini Ufaransa, yamezidi kuyeyuka baada ya mwanamichezo wake mwingine 'kuangukia pua' mwishoni mwa wiki iliyopita.

Licha ya kujitahidi, Sofia Latiff alishindwa kufua dafu katika mashindano ya kuogelea umbali wa meta 50. Binti huyo alishika nafasi ya mwisho katika kundi la tano.

Matokea hayo yalimwondoa Sofia katika orodha ya waogeleaji walioingia nusu fainali.

Sofia sasa ataungana na mwogeleaji mwenzake, Collins Saliboko kusubiri safari ya kurejea nyumbani.

Mwanzoni mwa michezo hiyo, Saliboko naye alishindwa kufanya vyema katika mashindani ya kuogelea upande wa wanaume katika umbali wa meta 200.

Saliboko alishika nafasi ya saba katika kundi la pili, akitumia muda wa sekunde 53.38 akishindana na waogoleaji wengine wanane.

Hata hivyo, Saliboko aliweza kuimarisha muda wake kwani muda aliotumia katika umbali huo unazidi ule alioupata wakati wa mashindano ya kitafuta nafasi ya kushiriki michezo hiyo.

Mshindi katika kundi hilo alikuwa Purahoo Ovesh kutoka Mauritius aliyetumia muda wa sekunde 52.22.

Awali, mcheza judo, Andrew Mlugu alishindwa kusonga mbele katika mchezo huo alipoondolewa hatua moja kabla ya kufika hatua ya robo fainali.

Hata hivyo, kushindwa kwa Mlugu kunatokana na kupata majeraha katika moja ya mapambano yake.

Matumaini ya Tanzania kupata medali katika mashindano hayo yamebakia kwa wakimbiaji wanne, Alphonce Simbu, Gabriel Geay, Magdalena Shauri, Jacline Sakiu ambao wanakimbia mbio ndefu.

Wanariadha hao wanatarajiwa kutupa karata zao wiki hii.

Kwa mara ya kwanza Tanzanai ilishiriki katika michezo ya Olimpiki maka 1964 iliyofanyika jijini Tokyo huko Japan.

Mwaka uliofuatia - 1965, mwanariadha Theresia Dismas aliipatia Tanzania medali ya kwanza ya michezo ya Olimpiki aliposhinda medali ya shaba katika michezo iliyofanyika Brazaville-Congo.

Mwaka 1968, mwanariadha John Akhwari alionyesha uzalendo wa hali ya juu ambao aliweka historia katika michazo hiyo pale alipojilazimisha kumaliza mbio za kilometa 42, licha ya kuumia. Licha ya kuachwa kwa muda mrefu na wanariadha wengine walioshiriki mbio hizo, Akhwari alihakikisha anamaliza mbio hizo huku akichechemea.

Alipoulizwa baadaye, aliwaambia waandishi wa habari kuwa hakutumwa na nchi yake kuja kushiriki, bali kumaliza mbio hizo.

Sifa kubwa kwa Tanzania katika michezo ya Olimpiki ilikuja mwaka 1980 pale mwanaridha wa mbio za kati, Filbert Bayi aliweka rekodi ya dunia ya mbio za meta 3,000.

Bayi pia aliweka rekodi ya kuwa Mwafrika wa kwanza kushinda mbio za kimataifa za umbali wa maili moja na meta 3,000.

# MICHEZO

Jumatatu, Agosti 5 - 11, 2024




Na Mwandishi Wetu



# Debora kuleta furaha Simba SC

KIUNGO Debora Fernandez Mavambo, anatabiriwa kuleta furaha katika klabu ya wekundu wa Msimbazi, Simba katika msimu ujao.

Hilo limejionesha wazi juzi usiku katika tamasha la 'Simba Day', ambapo kiungo huyo mwenye uraia pacha wa Congo ya Brazzaville na Angola kwa kufunga goli la kwanza ambalo lilizua shangwe kutoka kwa mashabiki wa timu hiyo.

Katika mchezo huo wa kirafiki, Simba iliibuka na ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya APR ya Rwanda katika tamasha la 16 la Simba Day kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam

Mabao ya Simba yalifungwa na kiungo mpya aliyesajiliwa kutoka Mutondo Stars ya Zambia, Debora Fernandez Mavambo dakika ya 46 na mshambuliaji, Edwin Charles Balua dakika ya 66.

## Yanga yang'ara

KATIKA kilele cha Siku ya Mwananchi jana, Yanga waliwafunza soka Timu ya Red Arrows kutoka Zambia kwa kuwafunga mabao 2-1.

Yanga ilifanikiwa kusawazisha bao, katika kipindi cha pili baada ya mchezaji wake, Mudathir Yahya, kupachika bao katika dakika ya 64. Red Arrows walipachika bao la kwanza dakika ya sita.

Wakati mashabiki wengi wakiondoka uwanjani, Aziz Ki, alitumia nafasi vyema kwa kufunga bao la pili kwa njia ya penati, katika dakika za nyongeza.


*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*